
TOLEO SEPTEMBA-OKTOBA 2023

# MUGAMBI




JARIDA LITAKALOTOLEWA KILA MWEZI NA IDARA YA UPASHANAJI HABARI

JIMBO KATOLIKI LA MUSOMA

S.L.P 93, Musoma –Tanzania

Somu: +255 754 076 709/0764 525 906/0755 893 303




# ASKOFU MSONGANZILA AZINDUA JUBILEI YA MIAKA 40 YA UPADRI



**Mwanga wa Kristo!** Naibu wa Askofu Padri Julius Ogolla akimkabidhi Askofu Michael Msonganzila Mshumaa kwa ajili ya kuzindua rasmi Jubilei ya Miaka 40 ya Ukuhani wake katika Kanisa Kuu la Maria Mama wa Mungu Siku ya Mshikamano Septemba 21, 2023. (Habari kamili na picha zaidi tazama ukurasa wa Pili).

## TAMKO LA MAASKOFU KATOLIKI TANZANIA


**Mkataba wa Uboreshaji Bandari za Bahari na Maziwa kati ya Tanzania na "Emirates of Dubai"**

# Tamko Lapinga Uwekezaji Bandari Zote

Bila kuumauma maneno Tamko hilo lililopewa Jina: **Sauti ya Watu Sauti ya Mungu** limeweka bayana kuwa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) haliungi Mkono Mkataba huo baada ya kuchanganua na kubainisha mapungufu yake. Tamko hilo limesainiwa na maaskofu 37 wakiwemo maaskofu wakuu 9 na Mwadhama Protas Kardinali Rugambwa na Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga, Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC).

Na Waandishi Maalum – Musoma

Endelea na Habari kamili Uk. 7



Mhashamu Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga, Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania, TEC

**Kutoka Uk wa 1:**

# AZINDUA MAANDALIZI YA JUBILEI YAKE



**Upendo Huvumilia Yote**: Hiki ni Kitenge cha Jubilei ya Miaka 40 ya Upadri wa Baba Askofu Michael Msonganzila



Baadhi ya matukio yaliyonogesha uzinduzi wa Jubilee ya Miaka 40 ya Upadrisho wa Mhasham Baba Askofu Michael Msonganzila



## Askofu Michael Msonganzila akionyesha hati maalum ya Upadri

Na Veronica Modest Musoma

Askofu wa Jimbo Katoliki la Musoma Michael Msonganzila amezindua rasmi maandalizi ya maadhimisho ya Jubilei yake ya miaka 40 ya Upadrisho na kuwaomba Waamini wa Jimbo hilo kuendelea kumuombea ili Mwenyezi Mungu aendelee kumtumza na kumpatia afya njema kwa ajili ya kuwachunga kondoo wake aliokabidhiwa.

Endelea Uk. 3

## TAHARIRI

Tunafarijika kuwaalika wadau wetu, waamini na viongozi wetu kuunga mkono jitihada zetu kwa kufuatilia "link" yetu na machapisho yetu yatakayozalishwa. Ni kwa kusambaza na kusoma machapisho yetu mintarafu Mugambi na tovuti ya Jimbo sisi tutapata nguvu ya kuendeleza kwa ujasiri, nguvu, weledi na ari mpya utume wetu wa upashanaji habari. Tunafahamu kusoma ni jambo moja na kuchangia maoni, makala na habari za matukio na picha ni jambo jingine. Sisi tunahimiza vyote.

Tumeshaanza safari na tumeamua kupiga hatua. Kwa mwendo wa haraka na uhakika tunakuja na mpango mikakati. Ni ndoto na matarajio yetu kuwa tutafika ikiwa tutaungwa mkono na wadau wa Jarida letu, wadau wa Idara yetu ya Upashanaji Habari na chaneli zetu za mawasiliano ikiwemo tovuti ya Jimbo na Mitandao yetu ya Kijamii mintarafu facebook na mingine itakayoibuliwa ili kutimiza ndoto ya Jimbo letu ya kwenda na wakati wa tehama.

Aidha, tunajua hizo ni kazi za kitaaluma. Tunajua ni kazi za vipaji na karama. Tunajua ni kazi za kujitolea na zenye msukomo na mhemko chanya kwa wadau wanaopendelea kujiendeleza, kutafuta maarifa na kuchangia maendeleo ya jambo hili kwa hali na mali. Lakini pia tunajua ni wito na maagizo ya Kanisa. Yesu mwenyewe aliwatuma Mitume wake "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe (Marko 16:15). Kwetu sisi, tunatimiza jukumu hili kwa kupasha habari njema.

Tuseme ukweli; Kanisa lenyewe ni chombo cha Habari Njema. Yesu Kristo, anaishi dunia ya leo wala asingekwepa kutumia vyombo vya habari. Ikiwa vyombo vya habari vinawafikia mabilioni ya watu kwa wakati mmoja, kwa muda mfupi...angekwepa vipi? Tunaamini angekuwa na twitter, linkedlin, tagged, facebook, skype, instagram, youtube na bado angeanzisha mtandao wake www. Habari njema/ YesuKristo.com. Au siyo?

Vivyohivyo angekuwa na vyombo vya habari vya kimataifa na mitambo ya radio na TV ya kutikisa dunia. Iweje leo, Jimbo letu likae kimya? Mitume wanaendelea kuhubiri watu wacheche bila kutumia nguvu ya vyombo vya habari? Tutawafikia lini watu wengi bila kutumia njia za upashanaji habari za kiteknolojia? Kwanini tusiseme tumeruhusu kupitwa na wakati? Dunia inaelekea kwenye teknolojia sisi tunaganda palepale? Je, tutalala hadi lini? Tunachelewesha Ufalme wa Mungu kwanini? Au tunakosea wapi? Watu wengi sasa wamejiunga na makundi sogozi wewe haumo kwanini? Watu wanawasiliana kwa mitandao wewe huna hata kiswaswadu! Unaishi karne ya ngapi? Lini Injili itafika pote kwa njia ya kisasa?

Idara yetu na taasisi zake tanzu inakuja na mpango kabambe wa miaka 10. Lengo ni kuchunguza fursa za kuwekeza katika mifumo ya kisasa ya kiteknolojia ya mawasilino na upashanaji habari ili kujibu mahitaji ya miaka 100 ijayo. Tunataka kuangalia mbele zaidi na kuweka msingi. Tunajiandaa kuwa na Kituo cha habari. Tunataka Televisheni, Radio na Wavuti. Siyo kwa kuota ndoto. Kwa dira na mipango. Kwa nini tushindwe? Kwanini hatuwezi kuota ndoto hizo?

Tunataka kupiga hatua. Chumba cha habari kinatakiwa kujitosheleza kwa mitambo na mifumo ya mawasilino ya kisasa yenye kuunganishwa na mkongo wa Taifa. Kiwanda cha uchapishaji cha digitali, mitambo ya kisasa ya kurekodi, kurusha matangazo na picha za video bila haja ya kuwa na kituo cha radio na TV (Podcast).

Bila kukurupuka, wenzetuwanapotembea sisi hatuna budi kukimbia tena tukiwa tunaelewa kuwa tumechelewa. Tunajua historia yetu, tulikuwa mbele kabisa na sasa tupo nyuma. Jimbo letu lilikuwa mfano likiogozwa na Mwanahabari wa kwanza tena mwasisi wa Idara ya Upashanaji Habari wa AMECEA (Pd Joe Healey MM).

Lakini hatukutumia fursa yake kwa manufaa makubwa licha ya jitihada zake ambazo zimerekodiwa vizuri. Tuliona Jimbo la Bukoba likisimama tangu awali na mwanzoni mwa miaka ya 1970. Wakasimika mitambo ya uchapishaji, wakaja na Gazeti la Rumuli na Tovuti na leo wana Radio Mbiu na bado wanapiga hatua.

Hatutakaa kimya. Tunapaswa kujiuliza na kuchukuwa hatua. Sisi tunakwama wapi? Leo tunataka matendo yazungumze zaidi. Tumeanza japo kwa kusuasua, tunaomba kuungwa mkono. Tutainuka na kuanguka. Lakini tuanze japo ni safari ndefu. Lakini tuanze. Twende tusajili, tuanze kuwekeza, kujitangaza, kukusanya habari, kuzichakata, kuhariri, kupata Kampuni ya uchapishaji au kununua mitambo na kutafuta fedha za uendeshaji na uchapishaji. Kuna mengi ya kutafakari na ndiyo maana tumeanza kufanya tafiti, kukusanya data na kuja na Mpango Mkakati wa Miaka 10. Katika Mpango huo tutabainisha mahitaji ya tasnia yetu, mkakati wa kuandika mchanganuo (Business Plan) na kubainisha vyanzo vya mapato ya kutegemeza mpango. Hatua zote zina safari ndefu na zahitaji raslimali fedha, kujitolea, zana za kazi, utulivu na vyanzo vya habari vya kuaminika bila kusahau sala, maombi na Baraka za Mungu.

Tunatarajia maombi ya waamini, mababa Paroko, Wakuu wa Idara, watawa na zaidi ni mchango wa mawazo, misaada ya hali na mali bila kusahau kufanya *"Subscription"* ya ***MUGAMBI na kuingia kwenye mitandao yetu ya kijamii***. Ni mwendelezo wa uinjilishaji kwa njia ya upashanaji habari - kwa kutumia machapisho na tehama. Tunakusihi utuunge Mkono!

*************************************************************



"Leo nimezindua rasmi Jubilei yangu ya miaka 40 ya Upadri. Kilele chake kitatangazwa rasmi na Kamati ya Kijimbo ambayo ndiyo inayohusika kupanga tarehe ya maadhimisho hayo mwakani, lakini kubwa ninalowaomba mapadri, masista, baba zangu, mama zangu wadogo zangu, na wajukuu wangu ,ndugu jamaa na marafiki ni Sala, maana bila Sala mimi mwenyewe siwezi kitu, hivyo niwakaribishe muungane nami katika Sala "amesisitiza Askofu Msonganzila katika hotuba yake.

Askofu Msonganzila ametoa ombi hilo wakati wa Misa Takatifu ya siku ya mshikamano kijimbo ambayo imefanyika Septemba 21, 2023, Kanisa Kuu la Maria Mama wa Mungu Musoma mjini, na kuhudhuriwa na waamini kutoka parokia zote za Jimbo la Musoma.

Askofu huyu amesema ameamua kufanya Jubilei hiyo ili kumshukuru Mungu kwa kumtunza hadi kufikia hatua hii kwani si kwamba katika Utume wake hakuna magumu ambayo hakuyapitia, yapo na ni mengi sana lakini kupitia maombezi ya Mama yetu Bikira Maria ameweza kufikisha miaka hii ya Utume na sasa anaona ni vema afanye sherehe ya kusema asante kwa Mwenyezi Mungu maana amefikia hatua hiyo si kwa mastahili yake binafsi bali ni kwa msaada wa Mungu kupitia Sala.

Akizungumza mara baada uzinduzi huo Naibu wa Askofu wa Jimbo hilo Padri Julius Ogolla amemshukuru Mhashamu Baba Askofu kwa kuzindua Jubilei hiyo ambapo amesema wanajimbo wako tayari kuungana naye Mhashamu Baba Askofu katika sala kwa ajili ya kusherehekea Jubilei hiyo, ili Mungu aendelee kumtunza kwa ajili ya kuchunga kondoo wake.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Walei Jimbo Katoliki la Musoma Costa Mniko amemhakikishia Mhashamu Baba Askofu kuwa walei wa Jimbo la Musoma wako pamoja naye katika Sala na wako tayari kuwapokea wageni wote watakaokuja kuungana na nao katika kusherehekea jubilei hiyo ya miaka 40 ya ukuhani kwani huo ni umri wa mtu mzima.

# HISTORIA IMEANDIKWA: KARDINALI WA TATU MTANZANIA ASIMIKWA RASMI.

Na Daniel Benno Msangya na Veronica Modest

**Baba Mtakatifu Francis amempa hadhi ya Ukardinali Askofu Mkuu Protase Rugambwa katika viwanja vya Mt.Petro Vatican Septemba 30, 2023 akiwa miongoni mwa maaskofu wakuu 21, waliopewa hadhi ya Ukardinali kutoka nchi mbalimbali duniani, watatu wakitoka Bara la Afrika. Mmoja wa maaskofu hao wakuu ni Protase Rugambwa, Askofu Mkuu Mwandamizi wa Jimbo Kuu Katoliki Tabora.**

Kardinali Rugambwa anakua Mtanzania wa 3 kupata wadhifa huu mkubwa baada ya Hayati Mwadhama Laurean Kardinali Rugambwa na Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo na sasa Mwadhama Protase Kardinali Rugambwa.

Kardinali Protase Rugambwa ni mzaliwa wa Karagwe, Jimbo la Kayanga, Kijiji cha Kasheshe, Parokia ya Katojo, kutoka ukoo wa Abakaraza (Abarigi). Majina yake ya kifamilia ni Protase Abakaraza.

Hilo jina la Rugambwa alipewa kama heshima kwa aliyekuwa Askofu Laurean Rugambwa ambaye alifanya ziara Bukoba siku aliyozaliwa Protase. Biblia inasema heri kuchagua jina jema kuliko mali nyingi (Mithali 22:1). Likawa jina rasmi.

Mapema Baba yake Protase alihama kutoka Karagwe akawa anafanya kazi Bukoba. Mama yake alipata ujauzito na Mei 31, 1960 alijifungua.

Siku hiyo Kardinali Laurean Rugambwa alifanya ziara ya kitume Bukoba. Baba yake mzazi, mtu wa imani na mfuasi wa dini Katoliki akasema kwa kuwa amezaliwa siku ambayo Askofu Rugambwa (kabla ya kutawazwa kuwa Kardinali) amekuja kwetu, basi utaitwa Rugambwa kwa jina lake.

Basi akabatizwa na kuitwa Protase Rugambwa. Na kama ambavyo jina hubeba tabia za mtu, hatimaye naye amekuwa Kardinali kama mtangulizi wake na somo au wajina wake.

Wazazi wapeni watoto wenu majina mazuri kabla ya kuwapa urithi wa mali. Inawezekana kwa wazazi kupata somo kwa kuwapa watoto majina mazuri.

Katika kuonesha mtangamano wa Kanisa (Church compatibility) Askofu Rugambwa amesindikizwa Vatican na viongozi mbalimbali wa Kanisa Katoliki na madhehebu mengine ya Kikristo. Mmojawapo ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Dayosisi ya Karagwe, Dkt Benson Bagonza (PhD) ambaye amekwenda Vatican kushuhudia tendo hili kubwa kwa mwana Karagwe mwenziwe.

Askofu Bagonza alipopewa nafasi ya kusema neno kuhusu Kardinali Rugambwa amesema "Ni mtu ambaye hekima imemzidi kimo na utu umemtangulia mbele. Ni Mnyenyekevu lakini si Mdhaifu. Mwenye nidhamu lakini si muoga."


Naye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan amempongeza Mwadhama Protase Kardinali Rugambwa kwa kusimikwa kwake rasmi na Kiongozi wa juu wa Kanisa Katoliki Duniani Papa Francis kuliongoza Kanisa la Tanzania.

Katika Salamu zake za Pongezi Rais Samia Suluhu ameonesha kufuatilia kwa karibu tukio hilo lililofanyika kwenye viwanja vya Kanisa Kuu la Mtakatifu Petro, Jijini Vatican, Roma kwa kuwavisha makadinali wapya kofia nyekundu na mahususi ya kutambua hadhi yao kama washauri wake wa karibu. Makardinali ndio Washauri wakuu wa Papa.

> Katika salamu hizo, Rais Samia alinukuu Injili ya Marko 16:15 "*Enendeni Ulimwenguni kote,*" (ikiakisi mafundisho ya Yesu Kristo kuhusu utume unaowajali watu wote, sehemu zote na wakati wote."

Rais ameandika katika mtandao na kukaririwa katika salamu zake wakati wa maadhimisho ya Sikukuu ya Jubilei ya miaka 125 ya Jimbo Kuu la Songea zilizowasilishwa na Waziri Mkuu Majaliwa Majaliwa. Katika salamu hizo Rais aliandika na kurejea kauli mbiu ya utume wa Kardinali Rugambwa, *"Euntes in Mundum Universum", yaani* "Enendeni ulimwenguni kote (ikiakisi mafundisho ya Yesu Kristo (Injili ya Marko 16:15) kuhusu utume unaowajali watu wote, sehemu zote na wakati wote." Alisema Rais Samia Suluhu na kuongeza kuwa anaungana na Watanzania wote kumtakia heri, afya njema na mafanikio katika utumishi wake.

Tumuombee Kardinali Rugambwa katika wajibu wake huu mpya wa kuwa Mshauri wa Papa. ***Roma Locuta, Causa Finita. Roma ikishasema, mjadala unafungwa"***



Mwadhama Protase Kardinali Rugambwa, Askofu mkuu Mwandamizi wa Jimbo kuu la Tabora Tanzania: Jengeni utamaduni wa umoja na mshikamano kama sehemu ya ujenzi wa Kanisa la Kisinodi na Ufalme wa Mungu (ANSA).

# JENGENI UTAMADUNI WA UMOJA NA MSHIKAMANO

## - ASEMA MWADHAMA PROTASE KARDINALI RUGAMBWA

**KARDINALI PROTASE RUGAMBWA AWATAKA WATANZANIA WAWE TAYARI KUJENGA NA KUDUMISHA UTAMADUNI WA UPENDO NA MSHIKAMANO NA WATU WENGINE HATA AMBAO SI WATANZANIA KAMA SEHEMU YA MCHAKATO WA UJENZI WA KANISA LA KISINODI. HUU NI MWALIKO WA KUENDELEA KUJIFUNZA KUJENGA UMOJA, USHIRIKI NA UTUME WA KANISA, ILI WATU WOTE WAWEZE KUFURAHIA MAISHA NA KUSHIRIKI KIKAMILIFU KATIKA UJENZI WA UFALME WA MUNGU HAPA DUNIANI. ANASEMA, TANZANIA KUMENOGA! KARIBUNI NYOTE!**


**Na Padre Richard A. Mjigwa, C.PP.S. – Vatican.**

Ni katika asili ya watu wa Mungu, Roho Mtakatifu ametenda kazi ya kutangaza na kushuhudia Fumbo la mateso, kifo na ufufuko kwa Kristo Yesu kwa wafu, Fumbo ambalo limewafikia watu wa Mataifa katika lugha zao za asili, kupitia kwa wazazi, makatekista, mapadre, wamisionari bila kuwasahau mabibi na mababu. Makardinali wapya wanaitwa na kutumwa kuwa ni wainjilishaji, kwani wao wameinjilishwa kwanza, tayari kupyaisha kumbukumbu na zawadi ya imani. Baba Mtakatifu Francisko katika Dominika ya Julai 9, 2023 aliwateuwa makardinali wapya 21 kati yao Makardinali watatu ni wale ambao wamejipambanua katika huduma kwa Kanisa na watu wa Mungu katika ujumla wao. Makardinali wapya wamesimikwa rasmi katika mkutano wa kawaida wa Makardinali wa Septemba 30, 2023 mjini Vatican. Baba Mtakatifu katika mahubiri yake amekazia zaidi uwakilishi wa Makardinali toka sehemu mbalimbali za dunia, kama ilivyokuwa siku ile ya Pentekoste ya kwanza, hawa ni Makardinali na Maaskofu wa nyakati hizi, ili kugundua kwa mshangao zawadi ya Injili waliyoipokea katika lugha zao wenyewe, tayari kumtangaza na kumshuhudia Kristo Yesu aliyeteswa, akafa na kufufuka kwa wafu; tayari kusimama kidete na kuwa ni wainjilishaji, huku wakimwilisha ndani mwao, ujenzi wa Kanisa la Kisinodi pamoja na kuendelea kumwaminia Roho Mtakatifu anayetengeneza utofauti na umoja; kiongozi mpole na thabiti.



Makardinali wanaitwa na kutumwa kuwa ni mashuhuda wa uinjilishaji mpya.

Mara baada ya Ibada ya kusimikwa kwa Makardinali wapya, Jumuiya ya Watanzania wanaoishi nchini Italia, ilimkaribisha Kardinali Protase Rugambwa, Askofu mkuu mwandamizi wa Jimbo kuu la Tabora kwa hafla ya "kufa mtu." Hii ni hafla iliyohudhuriwa na baadhi ya Maaskofu walioandamana na Kardinali Protase Rugambwa kutoka Tanzania pamoja na wageni waalikwa kutoka ndani na nje ya Italia. Mama yake Kardinali Protase Rugambwa ni kati ya waamini waliokuwa wamesheheni furaha kutoka katika sakafu ya moyo wake, aliposhuhudia Askofu mkuu mwandamizi Protase Rugambwa, akiwa miongoni mwa Makardinali wapya waliosimikwa na Baba Mtakatifu Francisko kwenye Uwanja wa Kanisa kuu la Mtakatifu Petro mjini Vatican. Katika mahojiano maalum na Radio Vatican, Mama Immakulata anakiri kwamba, kwa hakika, hii imekuwa ni siku yake ya furaha tangu kuzaliwa kwake, anaendelea kuamini uwepo angavu wa Mwenyezi Mungu katika maisha yake na kwamba, Mwenyezi Mungu amemtendea makuu na jina lake lihimidiwe. Hakutegemea kwamba, angeweza kumzaa mtoto ambaye baadaye amekuja kuwa ni Kardinali na hivyo kuheshimishwa ulimwenguni kote! Anamshukuru Bikira Maria na anamwomba, aendelee kumwombea Kardinali Protase Rugambwa ili awe na nguvu, imani thabiti na upendo kwa watu wote wa Mungu. Anawaombea akina mama wote waendelee kujikita katika malezi na makuzi bora ya watoto wao na kuwapatia nafasi ya kujiunga na seminari ili hatimaye, waweze kumtumikia Mungu na jirani zao kama Kardinali Protase Rugambwa. Wampende Mwenyezi Mungu na kudumu katika ushirika wa Fumbo la Utatu Mtakatifu.



**Kardinali Protase Rugambwa, Askofu mkuu mwandamizi wa Jimbo kuu la Tabora**

Kardinali Protase Rugambwa katika hotuba yake amewashukuru wote waliobahatika kujumuika kumpongeza pamoja na kumtakia heri na fanaka katika maisha na utume wake, tangu siku ile Baba Mtakatifu Francisko alipotia nia ya kuwatangaza Makardinali wapya ishirini na moja. Kwa hakika, wamekuwa ni msaada mkubwa kwake: kiroho, kimwili na ki-hali. Kardinali Protase Rugambwa, anamshukuru Mwenyezi Mungu pamoja na Baba Mtakatifu kwa yote anayomtendea katika maisha yake. Anawashukuru wale wote waliofika mjini Vatican kuhudhuria tukio hili kubwa katika historia ya maisha na utume wake na hivyo kuongeza nguvu katika Kanisa kwa kuwa ni wasaidizi na washauri wa karibu wa Khalifa wa Mtakatifu Petro. Kardinali Protase Rugambwa, anawaomba watu wa Mungu kuendelea kumkumbuka na kumwombea, ili sala zao ziendelee kumsindikiza katika maisha na utume wake kama Askofu mkuu mwandamizi wa Jimbo kuu la Tabora na kama Kardinali. Ameishukuru na kuipongeza Jumuiya ya Watanzania wanaoishi nchini Italia na kuwataka Watanzania kujenga na kudumisha: umoja, upendo na mshikamano wa kitaifa, mambo msingi yanayowatambulisha Watanzania, licha ya tofauti zao msingi. Wawe tayari kujenga na kudumisha utamaduni wa upendo na mshikamano na watu wengine hata ambao si Watanzania kama sehemu ya mchakato wa ujenzi wa Kanisa la Kisinodi. Huu ni mwaliko wa kuendelea kujifunza kujenga umoja, ushiriki na utume wa Kanisa, ili watu wote waweze kufurahia maisha na kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa Ufalme wa Mungu hapa duniani. Kardinali Protase Rugambwa, ametumia fursa hii, kuwakaribisha watu wote wa Mungu nchini Tanzania kwani "nyumbani kumenoga."



Rais Samia Suluhu Hassan amemtumia Kardinali Protase Rugambwa, salam za pongezi



*Balozi Mahmoud Thabit Kombo, Balozi wa Tanzania nchini Italia*

Balozi Mahmoud Thabit Kombo amesema kwamba, viongozi wa dini ni sehemu muhimu sana ya jamii katika muktadha wa ukuaji na ustawi wa maendeleo ya nchi sanjari na utambulisho wa wananchi husika. Amemtakia Kardinali Protase Rugambwa heri na baraka tele katika maisha na utume wake kama Askofu mkuu mwandamizi wa Jimbo kuu la Tabora. Amewashukuru na kuwapongeza wale wote waliojisadaka kuandaa "hafla hii ya kukata na shoka". Kwa namna ya pekee amewapongeza Watanzania kwa moyo wa uzalendo, moyo wa sadaka na majitoleo sanjari na kuendelea kujenga na kudumisha umoja na mshikamano wa Watanzania kitaifa. Amewasihi viongoni wa Kanisa waendelee kuliombea Taifa la Tanzania na viongozi wake ili waweze kutimiza malengo na ahadi zote za maendeleo kwa Watanzania. Na kwa upande wa viongozi wa Kanisa, waendelee pia kutekeleza ahadi zao kwa Kanisa. Balozi Mahmoud Thabit Kombo amesema kwamba, huu ni wakati wa kujenga na kudumisha umoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Afrika katika ujumla wake.

14.2. Ibaraya 4: inayohusu wigo wa Mahusiano na Utekelezaji unaoitaka Serikali ya Tanzania kuwajibika kuijulisha Dubai kila fursa ya uwekezaji inapojitokeza.Hiiinakinzana na baadhi ya sheria za nchi yetu, kwa mfanosheria ya ushindani na ile ya manunuzi.

14.3. Ibaraya 5: ambapo DPWorldimepewa haki ya kuendeleza, kusimamia na kuendesha miradi pekee yake, wakati Tanzania inabaki na wajibu wa kumwezesha kufurahia haki hiyo.

14.4. Ibaraya 6:inayoitaka Tanzania kuwajibika kuipatia DP World vibali na vivutio vya kutekeleza miradi yake kama Serikali. Hii inapingana na baadhi ya sheria za kiutaratibu.

14.5. Ibaraya 7: inayoitaka Serikali kuwajibika kutoa mamlaka yanayotakiwa na mwekezaji bila ucheleweshaji.

14.6. Ibaraya 8: Haki ya kutumia ardhi ambapo Mkataba unasababisha uvunjifu wa sheria za ardhi na sheria zinazohusu masuala ya ardhi.

14.7. Ibaraya 10: Usiri wa Mkataba ambapo Mkataba unazuia mamlaka nyingine kama TAKUKURU /BUNGE kufuatilia mikataba.

17. **Hivyo tukiwajibika kimaadili, tunaona ni jukumu la serikali kusikiliza wananchi wanaotaka mkataba huu ufutwe. Kwa kuwa tumeonesha kuwa Tanzania tumeshawekeza na kuendeleza bandari, reli na bandari za nchi kavu; niwajibu miradi hii tuiendeshe Watanzania wenyewe huku tukikaribisha ubia tunaoudhibiti wenyewe. Hiki ndicho wananchi wanachokililia kusudi tujenge uwezo wetu wenyewe. Kwa vile tumegundua mapungufu yetu ya uendeshaji wa bandari, tunaweza kujizatiti kurekebisha mapungufu hayo wakati njia za kiuchumi zikibaki mikononi mwetu. Kwa sababu hizo na maelezo yote ya hapo juu, sisi Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania hatuungi mkono Mkataba huu.**

Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania.

6

Ibara nyingine hatari zimetajwa (Namba 23 na 24) zenye ugumu wa kujitoa kwenye Mkataba.

Katika hitimisho lake, Tamko linaweka msisitizo na kusihi Serikali kutumia hekima na busara kuwasikiliza wananchi, "Maana kutokuwasikiliza ni kujiletea matatizo makubwa zaidi siku za usoni kwani wananchi hawa hawa watavitaka vijazi vijavyo kuondokana na unyonywaji huu, kama tunavyoona kwenye kesi nyingi zinazoendelea katika mahakama za kibiashara za kimataifa dhidi ya mikataba iliyovunjwa na Serikali ya Tanzania. Tukumbuke mikataba ya madini miaka ya 90 viongozi wa kidini na asasi za kiraia walipinga uwekezaji wa aina hii na Serikali ikatumia mamlaka zake kuridhia mikataba ya aina hii na sasa hivi tunashuhudia ikivunjwa na kugharimu Serikali kwa kulipa fidia kubwa.

16. Tunasisitiza kwamba **SAUTI YA WATU NI SAUTI YA MUNGU**, hivyo basi kuwasikiliza wananchi na kufanya maamuzi kadiri wanavyotaka kutailetea serikali heshima kubwa ya kuwa sikivu kwa watu. Kinyume cha haya, Mwenyezi Mungu anatuonya kupitia Nabii Yeremia anaposema: "*Kama kapu lililojaa ndege walionaswa, ndivyo nyumba zao zilivyojaa mali za udanganyifu. Ndiyo maana wamekuwa watu wakubwa na matajiri, wamenenepa na kunawiri. Katika kutenda maovu hawana kikomo hawahukumu yatima kwa haki, wapate kufanikiwa, wala hawatetei haki za maskini" (Yeremia 5:27-28).*

Imetolewa Dar es Salaam,

Tarehe 18 ya Mwezi Agosti Mwaka wa Bwana 2023.




Mhashamu Askofu Mkuu Gervas Nyaisenga
Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania.

Pd. Charles Kitima
Katibu Mkuu wa Baraza.

# Sista Mary Reese Mtukuka Hayupo Nasi Kimwili

**Na Daniel Benno Msangya**
Mwanahistoria na Mwandishi wa Kitabu cha Historia:
*Safari ya Imani; Kanda ya Ziwa Nyanza*

**Toleo lililopita tuliweka ahadi ya kumulika historia ya Jimbo la Musoma, kazi za kichungaji na huduma za kijamii za wamisionari.** Lengo ni kutoa ushahidi wa kimethali; kudhihirisha ukweli kuwa ***Vinavyoelea Vimeundwa***.



Tutawakumbusha waamini Mambo Yalivyoanza: Yaliyofanyika, Tunakotoka na Tulipo. Bila kusahau kuchambua nani alifanya nini, mchango wake na shirika lake. Leo tunaanza kwa tanzia.

Tutakosa ucheshi na tabasamu la kudumu lililofichuwa moyo wa ujasiri, ukarimu na upendo wa Sista Mary Reese MM., aliyetimiza miaka 101 kabla ya kutengana na dunia Agosti 20, 2023 huko kwao New York, Marekani. Septemba mwaka jana akiwa na rafiki yake kipenzi Sista Rosalie Lacorte, MM, wote masista wa Maryknoll (Tamka ***Merino***), Marekani aliadhimisha siku ya kuzaliwa (HBD) ya mwisho kabla ya kuitwa kupokea taji lake huko peponi katikati ya mwezi Agosti mwaka huu. Mapema Sista Rosalie mwenye asili ya Ufilipino alituma salamu za kufurahia tukio la sherehe ya kuzaliwa Sista Mary Reese iliyokuwa gumzo katika mitaa ya Kituo cha masista wa Maryknoll huko New York na kutangazwa hadi kwenye mitandao ya kijamii. Alikuwa ametimiza miaka 76 ya utume wake ndani ya Shirika la Masista wa Maryknoll na miaka 100 ya uhai na sehemu kubwa ya usichana na umama wake akiwa amejitolea sadaka kwa Waafrika kwa huduma za kichungaji na uuguzi. Safari yake ya Imani imetukuka tangu kuzaliwa na tangu mwaka 1945 akiwa msichana mrembo wa miaka 24.



MARAI… NDANI YA SUTI YA KIJIVU) NA SISTA ROSALIE LACORTE (KUSHOTO) WOTE MM.

Alijiunga na Jeshi la Marekani Kikosi cha Wauguzi (Army Nurse Corps) na kulitumikia katika Ukanda wa Bahari ya Pasific kwa mwaka mmoja hadi Agosti 1946 baada ya Vita Kuu *ya Pili. Kama walivyofanya vijana wengi waliotoka* jeshini mwaka uliofuata alijiunga na Shirika la Utawa la *Merino na kukutana na wanajeshi wenzake waliojiunga na mashirika ya Kimisionari akiwemo Padre John Casey (Kesi), Pd.John Hudert (Obong'o) na wengine waliotumikia Jimbo la Musoma katika Parokia za Muhoji, Tatwe, Ingri na Zanaki.*

Kazi yake ya kwanza ya umisionari alianzia Tanganyika ambako alitumwa na Shirika lake kuendeleza huduma za umisionari na uuguzi kwa miongo mitano hadi 2010 alipowaaga Watanzania na kurejea kwao Marekani kukamilisha sehemu ya mwisho ya utume wake katika Nyumba ya Kutunza Wazee, New York, Marekani.

Hata huko kwao kila mtu anamfahamu kwa ukarimu, ucheshi, moyo wa upendo uliofunuliwa kwa tabasamu lake kwa kila mtu aliyekutana naye. Sehemu ya Mswada wa Kitabu cha Msangya inasema aliponukuliwa katika mahojiano maalum mwaka 2008 (Safari ya Imani, 2023). Mwanamke mkakamavu aliyetumia pikipiki ya Honda (One 10) akiwa na umri wa miaka 80. Siri yake ni mazoezi na ukakamavu wa kijeshi. Alichapa kazi bila kujihurumia.

Mary Reese alizaliwa Desemba 8, 1922 huko Wilmington, DE kwa wazazi Elizabeth Reese na James Reese akiwa miongoni mwa watoto saba (wasichana wanne; Mary, Betty, Catherine na Cecilia na wavulana watatu wote watumishi kwenye altare ya Bwana, wakiwemo mapadre wawili - Charles na James na Monsinyori Thomas. Mary Reese alisoma Ursuline Sekondari na kuhitimu kidato cha sita mwaka 1940. Alijiunga na Chuo cha Uuguzi cha Mt. Francis na kutunukiwa stashahada ya Uuguzi mwaka 1943 na kujiunga na jeshi la nchi hiyo katika kipindi cha Vita Kuu ya Pili ya Dunia, akihudumu kama muuguzi wa majeshi.

Baada ya vita alijiuzulu jeshini na kuomba kujiunga na Shirika la Kimisionari la *Merino* Oktoba 5, 1946 na Aprili 6, mwaka uliofuata aliweka nadhiri za kwanza na Aprili 6, 1952 aliweka nadhiri za pili za maisha kwenye Kituo cha Masista, hapo New York.

Alitumwa kusomea shahada ya kwanza ya Sayansi ya Uuguzi katka Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Washington, DC mwaka 1950 na kujiendeleza kwa kozi ya ukunga katika chuo kingine cha Kikatoliki cha Santa Fe, NM na kupata cheti cha ukunga mwaka 1953. Utumishi wake alianza kwa mazoezi hapo kwenye Kituo, Kitengo cha Afya na baadaye mwaka huo 1953 alitumwa Afrika kwenye zahanati ya Kowak katika Jimbo la Musoma. Alifanya kazi za uuguzi na ukunga kabla ya kuhamishiwa Nassa na **baadaye katika hospitali ya Serikali Mkoani Mwanza. Mary** Reese alirejea kwao Marekani na kujiunga na Chuo Kikuu Maryknoll, New York ambapo mwaka 1974 alipewa Shahada ya Uzamivu ya Sanaa katika Teolojia.

Baadaye alihamishiwa Kenya na kufanya kazi katika Hospitali ya Kinango karibu na Mombasa akiwa muuguzi mwandamizi. Mwaka 1975 alirejea Tanzania na mwaka 1995 alianzisha harakati za mapambano dhidi ya Virusi vya Ukimwi, ugonjwa uliokuwa hatari na tishio kwa mamia ya maelfu ya watu katika Jimbo la Musoma. Alianzisha Kituo cha Vijana, Yatima na Watoto wanaoishi katika mazingira magumu bila kuacha watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi. Kituo hicho kilifanya mageuzi mwaka 2008 na kuitwa Kituo Hai cha Jamii (Community Alive Centre) kinachoendeleza mapambano hayo hadi leo kikihudumia watoto zaidi ya 300 kwa kuwawezesha kielimu kwa maendeleo yao siku za usoni na kuendeleza misaada ya hali na mali kwa wanaume na wanawake kwa kupewa mbinu za kukabiliana na changamoto za maisha yao ili waweze kuishi kwa matumaini.

**Sista Mary Reese atimiza miaka 100 akiwa na rafiki yake Sista Rosalie Lacorte, hatimaye kifo kimewatenganisha marafiki hawa.**



ALIHUBIRI KWA UKARIMU NA UPENDO KWA VITENDO. SR ROSALIE AKIWAPAKATA NA KUWAKUMBATIA WATOTO WENYE MAHITAJI MAALUM. JE, LEO WATOTO KAMA HAWA WANAHUDUMIWAJE AU HAWAPO?

Huku akisaidiwa na rafiki yake Sista Rosalie Lacorte waliyeshirikiana kwa muda mrefu katika miradi ya kuhudumia watoto yatima na walioishi na virusi vya Ukimwi, wengi wakiwa yatima. Baada ya muda wao kutimia masista wote waliagwa kwa huzuni na kurejea kwao mwaka 2010 na kujiunga na Jumuiya ya Masista wa Maryknoll wastaafu kwenye Kituo cha Jamii cha Rogers ambako walipangiwa majukumu mapya ya ibada, ushauri na kuhamasisha wamisionari vijana na kuwatia moyo.

## SISTER ROSALIE LACORTE BADO ANADUNDA

Katika hatua nyingine rafiki kipenzi wa Hayati Sr Mary Reese ni Sista Rosalie Lacorte aambaye anatimiza miaka 86 tangu alipozaliwa Aprili 4,1937 huko Lipa, Ufilipino kwa Mama Felisa Marquez Locarte na Bwana Rosendo Locarte. Sista Rosalie alizaliwa na msichana mwenzake mmoja katika familia hiyo. Rosalie alisoma katika shule ya Bibi Yetu wa Rozali Takatifu, Lipa na kuhitimu elimu ya sekondari 1955 na kujiunga na elimu ya juu katika Chuo cha Maryknoll katika Jiji la Quezon, Ufilipino ambako alipata shahada ya kwanza ya elimu msingi ya sayansi mwaka 1959. Alitumikia kama mratibu wa shule ya Maryknoll ya Mt.Bosco huko Suriago na baadaye mkuu wa shule hiyo huku alihusika na ufundishaji na idara ya ukatekesi katika eneo hilo.

Juni mosi, 1962 Rosalie alijiunga rasmi na Shirika la Masista wa Maryknoll huko Ufilipino na kuweka nadhiri za kwanza Machi 19, 1965 na nadhiri za daima Juni 9, 1971 huko huko Ufilipino.



SR. ROSALIE LACO
MWASISI WA TUPENDANE

Miaka 10 baadaye Sista Rosalie alitumwa kufanyakazi ya umisionari katika Jimbo la Musoma, Tanzania ambako alifanya kazi chini ya idara ya kichungaji na kuwahudumia wanawake. Ni wakati huo alipokuja na wazo la kuanzisha Kituo cha maendeleo ya kinamama kilichopata umaarufu kwa kuitwa TUPENDANE SENTA. Kituo hicho kiliendelezwa kufikia uwezo wa kujenga Kiwanda (Tupendane Cottage Industry). Kituo kilianza na wanawake vijana, wengi wakiwa wanatoka katika mazingira magumu na yatima.

Awali walianzisha darasa la kujifunza ufundi stadi wakitengeneza kadi, wakifuma masweta, sare za shule, mikufu na shanga, mavazi ya makasisi na mapambo. Walijengwa kwa mafunzo yaliyolengwa



kuwategemeza na kujitegemea. Baadhi ya wasichana hawa wakiwa yatima waliotokana na athari za Ukimwi, walikuwa wanalea watoto na wadogo zao katika mazingira magumu ya umaskini.

Walihitaji msaada na kuanzishwa kituo hicho ilikuwa fursa ya kuwaweka pamoja na kupokea msaada wa mafunzo na ujasiriamali. Walipokea mikopo na kuzalisha bidhaa ambazo waliuza kwa manufaa yao.

Ni katika kiwanda hiki kidogo ndipo Sista Rosalie alipanua huduma za mafunzo na kuonesha vipaji vyake vya ufundi wa kila aina huku akiwapa maarifa wasichana na wanawake vijana katika ufundi wa kushona, kufuma, kupika, lugha ya Kiingereza na biashara ya kutengeneza na kuuza majeneza! Aliwafunza pia kutunza mahesabu, kupanga bei, kufanya tafiti na kuanzisha na kuandika miradi ya mikopo midogo midogo yenye masharti nafuu.

Mafunzo hayo yalifanyika kwa nadharia na vitendo wakajishughulisha na miradi hai iliyowaingizia kipato na kuwaondoa kwenye umaskini wakimudu kujitegemea na kutegemeza familia na wadogo zao. Baadhi ya wanawake walipelekwa kwa mafunzo ya juu na baadhi walirejea na kusaidia kufundisha katika Kiwanda na Karakana ya Tupendane.

Mojawapo ya faida ya wazi iliyoonekana ni kuwajengea uwezo wa kujitegemea, kuimarisha dhana ya kuwajibika na kujiendeleza katika maisha na kupambana dhidi ya changamoto za umaskini na maradhi zilizokabili jamii zao hapo awali. Katika hatua hii, Sista Rosalie alishirikiana na Sista Mary Reese ambaye alikuwa mhudumu mwandamizi aliyeasisi Kituo cha Kijamii cha Community Alive akijihusisha zaidi na watoto, vijana na watu wazima walioathirika kwa janga la virusi vya Ukimwi.

Sista Rosalie alikuwa mwalimu, mlezi na mshauri aliyewatia moyo vijana wa kike na hasa wanawake vijana wakiwemo walioachishwa masomo kwa kupata ujauzito, wajane na wale waliovunjiwa ndoa, waliolea watoto na kuhudumia wagonjwa wa Ukimwi; aliwahamasisha waliokata tamaa, aliwainua waliopondeka roho, aliwapa dhana ya ujasiri, kujitegemea, maadili na uongozi na kuwawezesha kujitegemea kiuchumi. Baada ya kipindi kirefu cha miongo mitatu hapa Tanzania akieneza upendo, huruma, ujasiri, uwajibikaji na umoja kwa injili na matendo, Sista Rosalie alitumwa kwenda makao makuu ya Shirika lake mwaka 2010 na kufanya kazi katika Kituo cha malezi ya masista cha Rogers ambako anaendelea na kazi katika idara ya maendeleo ya Shirika hilo huku akisafiri na kutoa mihadhara kwenye vyuo na makanisa juu ya uzoefu wake na utume wa Shirika la Maryknoll Barani Afrika.

## WANAWAKE ACHENI KUTUPA WATOTO - ASKOFU SANGU

Na Veronica Modest, Lamadi.



**Askofu Sangu akiwa amewabeba watoto waliookotwa wakiwa tayari wameanza kushambuliwa na sisimizi masikioni na sasa wanalelewa katika kituo cha watoto Lamadi .**

**Askofu wa Jimbo Katoliki la Shinyanga Liberatus Sangu amelaani vikali vitendo vya ukatili kwa watoto vinavyoendelea kwa baadhi ya akina mama hasa wanaojifungua watoto na kuwatupa, kitendo ambacho ni cha kinyama na hakifai mbele za Mungu.**

Askofu Sangu amelaani vitendo hivyo wakati wa Maadhimisho ya Misa Takatifu ya uzinduzi wa Grotto la Yesu wa Ekaristi katika Kituo cha kulelea watoto cha Bikira Maria Mama wa Mungu Msaada Daima, Lamadi, Busega ambapo amesema kujifungua na kutupa mtoto, "huo ni zaidi ya ukatili walio nao wanyama kwa kuwa sasa hivi binadamu hathamini kabisa suala la uumbaji,"alitetema na kuongeza,"inasikitisha sana kuona watoto wanakuwa balaa,chukizo na sio Baraka tena na nyakati hizi mambo yamekuwa mengi sana, kwani ukatili dhidi ya watoto ni mkubwa sana, watu wanahangaika kwa waganga kutafuta watoto ila sisi tunawakatili na kuwatupa.

Mkurugenzi wa Kituo hicho cha Kulea Watoto Sista Helena amesema Kituo kina watoto wengine huko Pugu, Mwanza, Lamadi na Musoma ambao wanapokelewa na kusaidiwa kulingana na changamoto mbalimbali wanazokuwa nazo, na wengine wamekuwa wakiwapokea wakiwa na hali mbaya. "Kadhalika wengine wanakufa kutokana na kuchelewa kupelekwa kituoni hapo baada ya kutupwa au kutelekezwa na wazazi wao."

"Hapana tusifanye hivyo, watoto wanaokotwa tayari wakiwa wameshaanza kushambuliwa na wadudu (sisimizi) na wengine wanathubutu kutupa watoto wakiwa bado hawajafikia umri wa kuzaliwa. Wanawake wanatoa mimba na kuwatupa chooni, nawaomba tuwe watetezi wa uhai wa binadamu," alisisitiza Askofu Sangu.

Amesema haijalishi mtoto huyo kapatikana kwa njia gani na kama Mama Bikira Maria angemtupa Yesu sijui ni nani angetukomboa tena kwa kutoa uhai wake, hivyo, tunapaswa kujifunza kutoka kwake kwani mtoto ni Baraka na sio laana. Tuwapokee na tuwalee kulingana na mafundisho ya Yesu,na huo ndio wajibu wetu kama Wakristo ambao kila mara tunasisitiza kutunza na kulinda uhai.

Sista Helena amesema Kanisa Katoliki linatetea uhai wa mwanadamu na hata mtoto anayetupwa au kutelekezwa na wazazi au familia ana chumba pale, kwani Yesu anasema wote wenye kuelemewa na mizigo wamfuate. Kwa kushirikiana na akinamama wanao msaidia kulea watoto hao, wako tayari kuwasaidia watoto wanaoteseka kuliko kufanyiwa ukatili na hata kupoteza uhai wao.

# WACHUMBA WAHIMIZWA KUCHUNGUZANA KABLA YA NDOA

Na Veronica Modest - Kiongera

**Watu wanaotarajia kuungana na kufunga pingu za maisha popote nchini wamekumbushwa kuchunguzana kwa kina na kwa muda mrefu kabla ya kufanya maamuzi ya kufunga ndoa ili kuwasaidia kuishi agano la Mungu kwa kuzingatia mwongozo wa Kanisa Katoliki unaosisitiza kutenganishwa na kifo.**



Baba Askofu Msonganzila akiwa na wanandoa na familia yao

Ndoa nyingi kwa sasa zimekuwa ni ndoano kulingana na wanandoa wengi kukutana ndani ya wiki moja na kufanya uchumba wa siku na miezi michache na kisha kufunga ndoa.

"Hali hiyo inasababisha ndoa nyingi kuvunjika mara baada ya kila mmoja kumfahamu vizuri mwenzake."

Hayo yamebainishwa na Paroko wa Parokia ya Tarime Jimbo Katoliki la Musoma Padri Lucas Chacha wakati wa Maadhimisho ya Misa Takatifu ya kumshukuru Mungu kwa kuwafikisha siku hiyo ya kutimiza miaka 50 ya ndoa ya Mzee Stanslaus Sabure na Maria Nyarugendo, Misa iliyofanyika nyumbani kwao katika Parokia Teule ya Kiongera na kuongozwa na Mhashamu Baba Askofu wa

Jimbo Katoliki la Musoma Michael Msonganzila, hivi karibuni.

Padri Chacha amesema kumekuwepo na changamoto kubwa sana ya kuomba kutengana mara baada ya kupokea Sakramenti ya ndoa hali inayoashiria maandalizi mabovu ya kipindi cha uchumba kabla ya kufanya maamuzi ya kuishi pamoja.

Akizungumza siri ya kufikisha miaka hiyo ya ndoa mzee Stanslaus Sabure ambaye ni baba wa Padri Cleophas Sabure wa Jimbo hilo amesema sio kwamba hakuna changamoto walizokutana nazo hadi kufikia siku hiyo,lakini moja ya siri kubwa ni kuvumiliana katika taabu na raha,lakini hasa ni upendo wa dhati.

Mzee Stanslaus Sabure amewashukuru wote waliofika katika kusherehekea jubilei ya miaka 50 ya ndoa, ambapo kwa miaka ya sasa ni ngumu sana vijana wengi kufikisha miaka hiyo na hata kujaliwa kufikisha umri wao.

"Nataka niseme ukweli. Katika migogoro mingi inayotuhangaisha maofisini kwa sasa ni migogoro ya wanandoa wakiomba kuachana, sasa unajiuliza hawa wana muda mfupi ndani ya maisha ya ndoa lakini kwa nini wanaomba kuachana, majibu unakuta kwamba uchumba wao waliufanya, aidha kwa njia ya mtandao au walikutana ndani ya miezi michache tu na kufanya maamuzi ya kuoana, na haya ndio matokeo yake," amesema Padri Chacha maarufu kwa lakabu ya Sokoro.

Amewaasa vijana wa sasa kuacha kuingia katika ndoa kwa sababu ya shinikizo la wazazi, ndugu na jamaa bali waingie baada ya kuchunguzana kwa muda na kuwashirikisha wazazi ili kuwasaidia kufuatilia mienendo ya maadili katika familia husika.





# MASONGA WAKUMBUSHWA KUZINGATIA MAADILI

Na Veronica Modest- Masonga.

**Wanafunzi wanaohitimu darasa la saba na kidato cha nne, wamekumbushwa kuhakikisha wanazingatia malezi na maadili mema waliyofundishwa walipokuwa shuleni na kuhakikisha wanayaendeleza ili kuwa mfano bora kwa jamii, lakini pia kuwa kioo katika kutangaza taasisi walizosomea kwa kuwa kioo cha jamii.**

Hayo yamesemwa na Padri Julius Magere Paroko wa Parokia ya Serengeti na Katibu wa Idara ya Elimu Jimbo Katoliki la Musoma, wakati wa mahafali ya 18 ya wanafunzi wa awali na darasa la saba wa shule ya Milenia ya tatu, Masonga, Jimboni humo na kumshukuru Mungu kuwafikisha siku hiyo baada ya kukaa shuleni kwa miaka zaidi ya 7 kuanzia elimu ya awali hadi ya darasa la saba kwa mwaka 2023.

Padri Magere amesema kwa muda wa miaka waliyokuwa shuleni wamekuwa na nidhamu na maadili mema ambayo yamekuwa kivutio kwa wengine, na kwamba taasisi za kanisa zimekuwa mfano wa kuigwa kwa malezi bora hivyo hawana budi kuyaendeleza ili kumtangaza Kristo katika matendo.

"Tunawashukuru wote kwa muda ambao tumekuwa wote na sasa mnaondoka katika taasisi zetu za elimu, haitapendeza tukisikia kuwa mtoto fulani aliyesoma katika shule fulani inayosimamiwa na kanisa anahusishwa na mambo maovu huko mtaani kama ya kulewa kupindukia, wizi, uvutaji wa bangi na madawa ya kulevya, hapana. Hatutaki kusikia hivyo. Kuweni mfano bora kwenu wenyewe na kwa taasisi zilizowapika hadi mkaiva kimaadili na kiroho,"amesema Padri Magere.

Padri huyo amewakumbusha wazazi pia kuwajibika kwa watoto ipaswavyo katika kipindi hiki ambacho sasa wanakwenda kukaa nao kwa muda wakisubiri matokeo yao ya mtihani ambayo wanaamini kuwa wote watafaulu kulingana na namna walivyofundishwa na kufanya mazoezi mengi, kuhakikisha wanatenga muda wa kutosha wa kukaa nao ili kuwafahamu watoto wao vizuri kitabia na kimwenendo na sio kuwaachia wenyewe wajilee bila kudhibitiwa.

Msimamizi wa shule hiyo, Sista Irene Loina Kaibunga wa Shirika la *Incarnate Word Sisters* ambao ndio wasimamizi wa shule hiyo amewashukuru wanafunzi na wazazi kwa kuwaamini na kuwaleta watoto wao katika Shule ya Milenia ya tatu Masonga kwani watoto wao wanapata elimu bora ya kiroho na kimwili, kwa kuzingatia maadili na tamaduni za Kitanzania.

Kaimu Afisa elimu awali na msingi Wilaya ya Rorya, Paulin Chacha ambaye alikuwa mgeni rasmi ameupongeza uongozi wa shule hiyo kwa kuwa ni moja ya shule ndani ya Wilaya hiyo inayofundisha vizuri maadili kwa kuzingatia mwongozo wa Serikali na mwongozo wa Kanisa, lakini katika ufaulu ni shule bora kwa kata ya Tai.

Kanisa Katoliki Jimbo la Musoma limetengeneza Sera ya ulinzi wa watoto ambayo inalenga kuwalinda, kuwatetea, kuwahudumia na kuwapa watoto haki za msingi ikiwemo elimu na mahitaji mengine ya kimaendeleo kiroho na kimwili,tayari yapo mapendekezo kuichapisha hapa katika toleo maalum au kwa vipande ili ieleweke na wadau na wasomaji wetu.

## HONGERENI KWA MSHIKAMANO WANAKIONGERA -ASK MSONGANZILA

Na Veronica Modest-Kiongera.

**Waamini wa Parokia Teule ya Kiongera Jimbo Katoliki la Musoma wamepongezwa kwa kuendelea kuwa na umoja, upendo na mshikamano katika kujiletea maendeleo katika Parokia yao, kutokana na kufanya mambo makubwa ya maendeleo ndani ya muda mfupi, baada ya kutangazwa kuwa Parokia Teule.**

Pongenzi hizo zimetolewa na Mhashamu Baba Askofu wa Jimbo hilo Michael Msonganzila ,wakati wa Maadhimisho ya Misa Takatifu ya Sakramenti ya Kipaimara kwa waamini zaidi ya 370 wa Parokia

hiyo,wakati wa ziara yake ya kichungaji katika Parokia hiyo hivi karibuni.
Askofu Msonganzila amesema kwa muda mfupi sana waamini wameweza kufanya mabadiliko makubwa ya kimaendeleo, hali inayoonesha ukomavu wa kiimani kwa waamini, lakini pia uaminifu katika kusimamia kile kinachopatikana kutokana na majitoleo yao.

"Naomba niwapongeze kwa moyo wa dhati kabisa,nimefurahi sana kuona mabadiliko haya makubwa, na haya yote yanatokana na mshikamano mlionao, bila umoja na mshikamano hakuna maendeleo yanayoweza kupatikana, endeleeni na umoja huo na Mwenyezi Mungu abariki kazi za mikono yenu,"amesema Askofu Msonganzila.

Paroko wa Parokia hiyo Padri Athanas Zengo, OSA amemshukuru Baba Askofu kwa kukubali kufika katika Parokia hiyo na kutoa Sakramenti Takatifu ya Kipaimara kwa waamini hao na kuwatia moyo katika Utume, na kwamba kufika kwake kunaongeza zaidi mwamko katika imani.

Padri Zengo amewashukuru pia waamini wote wa Parokia Teule ya Kiongera kwa mshikamano walionao katika kujitoa sadaka kwa kazi ya Mungu na kuwaomba kamwe wasirudi nyuma katika kumtolea Mungu sadaka, kwani majitoleo hayo ni hazina mbinguni.

# ACHENI KUBADILI MAJINA KABLA NA BAADA YA KUBATIZWA –ASKOFU MSONGANZILA

Veronica Modest, Mwisenge

**Askofu wa Jimbo Katoliki la Musoma Michael Msonganzila amekemea tabia ya baadhi ya waamini kubadili badili majina yao mara kwa mara baada ya kubatizwa kwa kisingizio kuwa majina ya awali yalikuwa sio ya mzazi sahihi na sasa ndio mzazi halisi amepatikana.** Onyo hilo limetolewa wakati wa Misa Takatifu ya ufunguzi wa jengo la ofisi ya Parokia ya Mtakatifu Agostino, Mwisenge Jimboni humo, iliyofanyika hivi karibuni ambapo amesema suala la kubadilisha badilisha majina limekuwa likileta kesi kubwa baina ya wazazi na watoto, hivyo ni vema mzazi wa kike akawa mkweli ili kuepusha usumbufu baadae.

"Kuna kesi za ajabu ajabu kweli, mtoto anazaliwa mama anatumia jina la baba anayemfahamu, baada ya mtoto kubatizwa na kuwa mkubwa, anaambiwa ukweli, anaanza kusema kuwa lile jina nililoandikwa kwenye kitabu cha ubatizo sio la baba yangu mzazi sasa ndio baba yangu mzazi

amejitokeza na hivyo naomba nibadilishe jina, hii hatutaruhusu kabisa ni usumbufu mkubwa,"amesema Askofu Msonganzila.

Askofu Msonganzila amesema Ofisi za Parokia ni sehemu muhimu katika kutunza taarifa mbalimbali za waamini ikiwemo kutunza vitabu vya fedha, mapato na matumizi, vitabu vya Ubatizo, Komunyo, Kipaimara, Ndoa, hali ya maendeleo ya Parokia husika pamoja na idadi kamili ya waamini na idadi ya jumuiya.

Paroko wa Parokia ya Mwisenge na Naibu wa Askofu wa Jimbo Katoliki la Musoma Padri Julius Ogolla amemshukuru Mhashamu Baba Askofu kwa kukubali kufika katika Parokia hiyo kwa ajili ya kuwafungulia Jengo la Ofisi ya Parokia, ambapo tangu kuanzishwa kwa Parokia hiyo hawakuwa na ofisi ya kisasa.



Padri Ogolla amesema suala la utunzaji wa nyaraka za parokia ni muhumu na kwa sasa wamepata sehemu muhimu ya kuhifadhi nyaraka na kuendesha huduma za kichungaji.
"Tunakushukuru baba licha ya kuwa na majukumu mengi ya kichungaji umekubali leo kusali nasi na kutufungulia rasmi jengo letu la ofisi, sisi wana Mwisenge tunasema asante sana na zaidi tunakuombea Mwenyezi Mungu aendelee kukupatia afya njema ya roho na mwili,"amesema Naibu Askofu Padri Ogolla.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya waamini, Mwenyekiti wa Parokia hiyo Benedicto Masatu amesema ujio wa Mhashamu Baba Askofu katika sherehe hiyo ya ufunguzi wa ofisi ya Parokia unaonyesha ni kwa jinsi gani baba anawapenda wanaye na kuamua kuja kushiriki nao katika furaha waliyonayo.

# AKINA MAMA SHIRIKISHANENI UBUNIFU KUKUZA KIPATO CHENU
## -ASKOFU MSONGANZILA



Hili ni jengo la Kitega Uchumi cha WAWATA.



Baba Askofu Michael Msonganzila akizindua rasmi jengo hilo hapo Kiabakari.

Na Veronica Modest, Musoma.

**Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA) wametakiwa kuwasaidia wanawake wengine katika kubuni miradi mbalimbali ya maendeleo ili kuwasaidia kuinua kipato chao cha familia na taifa kwa ujumla.**

Akizungumza wakati wa ufunguzi rasmi wa Jengo la Kitega Uchumi cha Wanawake Wakatoliki Kiabakari (WAWATA), Askofu Michael Msonganzila amewapongeza na kuwataka kufundishana mbinu mbalimbali za kujiingizia kipato na kuondokana na utegemezi ndani ya familia na hata ndani ya kanisa.

"Mama zangu washirikisheni wanawake wengine katika Parokia nyingine mbinu mlizotumia kupata wafadhili hadi mmefikia hatua hii kubwa," amesema Askofu Msonganzila.

Naye Paroko wa Parokia hiyo Padri Adam Wojciech amewashukuru akinamama wanne waliojitoa kwa ajili ya wanawake wengine hadi kufanikisha kupatikana kwa mradi huu mkubwa ambao utasaidia kuinua kipato cha akinamama na kuongeza ajira.

Akisoma taarifa ya mradi huo katibu Msaidizi wa WAWATA Parokia ya Kiabakari Flora Jacob amesema wazo la kuanzishwa kwa mradi huo lilifanikishwa baada ya Akinamama kumshirikisha Baba Paroko wao Padri Wojciech kuhusu hali duni ya kipato na kuja na wazo la mradi huo.

"Baada ya kuona hali duni ya kipato cha wanawake, ndipo tulipoamua kumshirikisha baba paroko ili atusaidie kupata wafadhili ambao wataweza kutujengea kitega uchumi cha kudumu kitakachopunguza hali ya umasikini katika familia zetu na kuondokana na utegemezi."Paroko aliamua kuwatafutia wafadhili kutoka nchini kwao Poland.

Wanawake hao wamemshukuru na wanamuombea maisha marefu na Utume mwema baba Paroko Wojciech kwa kuwasaidia kuwatafutia wafadhilia ambao wamejenga kitega uchumi hicho ambacho kitawasaidia mahujaji wanaofika katika Parokia hiyo kwa ajili ya Hija kila mara kupata huduma mbalimbali kama vile chakula, malazi, vinywaji, saluni na huduma za kifedha ambazo zitakuwa zinapatikana katika kitega uchumi hicho kinachoitwa: JUBILEE COMPLEX katika Parokia ya Huruma ya Mungu Kiabakari Jimbo Katoliki la Musoma. , Wameanza na kidogo wanachoweza kusimamia kulingana na mazingira na uwezo wao na wakati huo kujifunza na kujipatia uzoefu utakaosaidia kuongeza kasi ya uzalishaji mali, biashara na uboreshaji huduma kupitia kitega uchumi hicho.

## HABARI NA MAKALA KUTOKA MAJIMBONI

# WASHAURI MAPROFESA KUONGEZWA UMRI WA KUSTAAFU

**DODOMA: Maprofesa 161 wanahitajika katika Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam ili kuziba pengo la wahadhiri waandamizi linalokabili chuo hicho na kuhatarisha ubora wa taaluma katika taasisi hiyo ya elimu ya juu Afrika Mashariki.**

Waziri wa Elimu Profesa Adolf Mkenda amekiri kuwepo kwa upungufu huo mkubwa na kubainisha kuwa kwa sasa wapo Maprofesa tisa.

Alikuwa akijibu swali la wabunge waliotaka kujua Serikali inachukuwa hatua gani kunusuru taaluma inayotolewa na wahadhiri wenye hadhi ya uprofesa chuoni hapo. Aidha Wabunge waliiomba Serikali kuongeza umri wa maprofesa kutoka miaka 65 hadi 70 ili kupunguza kasi ya maprofesa wanaostaafu kwa mujibu wa umri.

Serikali katika maelezo yake ilifafanua kuwa Tanzania inao maprofesa 226 wakiwemo maprofesa kamili 63 na wengine washiriki 163 na kwamba katika mpango wa muda mrefu Serikali inatarajia kuandaa jumla ya vijana 600 watakaopelekwa kwenye mafunzo. Hata hivyo Waziri Profesa Mkenda hakueleza wanafunzi hao watapatikana kuanzia lini wakiwa na viwango vya elimu ya udaktari na uprofesa ili kuziba pengo la upungufu unaonyelemea vyuo vikuu vya Tanzania.

Kuhusu umri Serikali imesema itafanyia kazi suala la umri baada ya kuongeza umri wa kustaafu Profesa kutoka miaka 60 hadi 65 na kwamba mahitaji yanasukuma uamuzi huo wa kuongeza umri zaidi kufanyiwa kazi.

Hatua hiyo pia itahusisha maslahi yao duni ambapo Serikali itaangali maslahi ya watumishi wote wa vyuo vikuu. Katika hatua nyingine Serikali imepanga kushughulikia maslahi ya wadhibiti ubora wa elimu nchini na kwamba Serikali imeshakuja na muundo mpya wa mshahara kuanzia Julai 2023 ambapo badala ya – TGTS – sasa itatumia TGTSQ. Waziri huyo pia alisema idara ya kudhibiti ubora wa elimu nchini imepewa vifaa vya Tehama, vikiwemo vishikwambi 1680, computer mpakato 1002 na kuendeleza ujenzi wa ofisi 5 za wilaya kati ya halmashauri 181. Kuhusu mpango wa kuimarisha elimu katika sekta ya ukaguzi na udhibiti ubora, Serikali inasema inalenga kusogeza huduma hizo kutoka ngazi ya kanda kuje ngazi ya mikoa na wilaya na kuendeleza mafunzo ya umahiri. Je, hiyo ni mipango ya makaratasi kama ilivyokuwa sera ya elimu (2014)? Walihoji wabunge na kubainisha kero ya fedha za uchangiaji elimu (kero na usumbufu) kutokana na kubadili miongozo na kuchelewesha fedha kuwafikia wadhibiti ubora wa elimu. Bado kuna maswali mengi wajengewe uwezo ili wafanye miujiza gani ikiwa kwa mfano hadi sasa wanakagua nini wanapopitia madaftari ya mwanafunzi wa lugha ya Kiingereza shule ya msingi na sekondari? Wanajiridhisha vipi?

# MAHENGE WAZINDUA JUBILEI MIAKA 50 YA JUMUIYA NDOGONDOGO KWA KISHINDO

Barua ya Kichungaji kwa Taifa la Mungu Jimbo Katoliki la Mahenge: "***Gaudium Magnum***" yaani "Ni Furaha Kubwa" iliyotolewa na Mhashamu Askofu Agapiti Ndorobo, wa Jimbo Katoliki la Mahenge imebainisha kuhusu uzinduzi wa Maadhimisho ya Jubilei ya Miaka 50 ya Jumuiya Ndogo ndogo, na kusisitiza kuwa hiki ni kipindi cha kupyaisha imani kwa: Sala, Neno la Mungu na Sakramenti za Kanisa.

Mapema Agosti 20, 2023 Shirikisho la Mabaraza ya Maaskofu Katoliki Afrika Mashariki na Kati, AMECEA, lilizindua Maadhimisho ya Jubilei ya Miaka 50 ya Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo, huko Lilongwe, nchini Malawi na kufuatiwa na warsha ya siku tatu juu ya Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo pamoja na Ulinzi wa Mtoto. **"GAUDIUM MAGNUM" Ni furaha kubwa tunapotambua na kuona wazi kuwa Mwenyezi Mungu anatupenda.** Katika kutupenda, Mungu anatujalia nafasi ya kuyatafakari makuu anayotutendea katika safari yetu ya kiroho.

Wapendwa Taifa la Mungu, Kanisa Barani Afrika na kwa namna ya pekee kanda ya AMECEA linajipambanua kama familia ya Mungu.



*Baragumu ni sauti ya mwaliko wa kushirikisha watu wa Afrika. Hii ni mbiu ya mugambo, ikilia kuna jambo.*

Tunawatangazia rasmi Jubilei ya miaka 50 ya Jumuiya Ndogondogo za Kikristo. Maadhimisho ya jubilei hiyo yalianza rasmi mwezi Julai 2023 na kilele chake kitafanyika mwezi Julai mwaka 2024.

Kauli Mbiu inayoongoza maadhimisho hayo ni: "JUMUIYA NDOGONDOGO ZA KIKRISTO: MIAKA 50 YA KUJENGA KANISA KAMA FAMILIA YA MUNGU KATIKA NCHI ZA AMECEA." Katika Jimbo la Mahenge, uzinduzi wa maadhimisho hayo ulifanyika Julai 27, 2023 katika Kanisa Kuu la Kwiro.

Askofu Agapiti aliagiza kwamba: kila parokia kuandaa utaratibu wa uzinduzi rasmi katika ngazi zote yaani uzinduzi kiparokia, kivigango na kwa namna ya pekee katika Jumuiya Ndogondogo za Kikristo. "Tunapendekeza kwamba, katika parokia zote ambako hatujafika kwa ziara za kichungaji na utoaji wa Sakramenti ya Kipaimara, kufanyike maandalizi ya kuwezesha uzinduzi katika ngazi ya parokia au kigango husika uendane na tukio la utoaji wa Sakramenti Takatifu ya Kipaimara mwaka huu 2023." Aidha jimbo limeandaa utaratibu maalumu kwa zile parokia ambako Kipaimara kimeshatolewa kwa mwaka 2023.

Ifanyike tathmini ya kina juu ya mafanikio na changamoto tunazopaswa kuzifanyia kazi katika Jimbo letu la Mahenge. Yatolewe pia mapendekezo ya namna ya kuzitatua changamoto hizo kadri ya mazingira yetu.

Tunaaagiza kwamba tathmini hizo zitufikie kupitia Idara yetu ya kichungaji na zitajadiliwa kwenye mikutano yetu ya kichungaji jimboni. Wapendwa katika Kristo Bwana, tunaagiza kwamba:



Pyaisheni imani kwa njia ya Neno la Mungu na Sakramenti za Kanisa

**Katika Maadhimisho haya ya Jubilee ya Miaka 50 ya JNNK, kila parokia iandae utaratibu utakaowezesha kufanyika kwa mikutano maalumu ya kutafakari uhai wa jumuiya zetu na kwa namna** ya pekee kukuza uelewa wa watu juu ya dhana nzima ya JNNK.

SALA MAALUMU YA JUBILEI isaliwe na wanajumuiya wote wanapokutana pamoja kusali na kutafakari Neno la Mungu. Aidha, yatolewe mafundisho ya Imani na kuwahimiza waamini kuziishi kweli za Imani yetu hasa maisha ya Sakramenti hususani; NDOA TAKATIFU, SAKRAMENTI YA UPATANISHO NA EKARISTI TAKATIFU. Maadhimisho haya ya Jubilee ya Miaka 50 ya JNNK yatumike kama fursa muhimu ya kukuza Imani yetu na kuimarisha uhai wa Jumuiya zetu Jimboni Mahenge. Mapadre na watawa tushiriki katika mikutano hii muhimu.

**Wapendwa Taifa la Mungu, katika jimbo letu la Mahenge, sherehe za kufunga maadhimisho ya Jubilei hii ya miaka 50 ya JNNK yatafanyika mwezi Julai mwaka 2024**. Ndugu zangu katika Kristo, kwa waraka huu pia, tunawatangazia rasmi kwamba mwaka wa Bwana 2024 ni mwaka wa Ekaristi Takatifu. Hivyo kuanzia tarehe 8 hadi tarehe 15 mwezi Septemba kutakuwa na Kongamano la 53 la Kimataifa la Ekaristi Takatifu katika mji wa QUITO nchini EQUADOR. Aidha hapa nchini Tanzania kilele cha maadhimisho hayo kitafanyika katika Kanda yetu ya Mashariki katika Jimbo Kuu la Dar es Salaam. Tumwombe Mungu afanikishe shughuli zote za maadhimisho hayo muhimu na tujiandae kushiriki kwa hali na mali. Mwanzoni mwa mwaka 2024 kutafanyika uzinduzi rasmi wa maadhimisho hayo. Tutawatangazia tarehe rasmi ya uzinduzi huo," waraka wa Askofu Agapiti ulisisiza.

**MBIU YA MGAMBO IKILIA KUNA JAMBO:**
**Wanajumuiya Tunaalikwa Kutafakari na Kufanya Tathmini ya Mafanikio na Changamoto za Jumuiya Yetu Tangu ilipoanzishwa: Ni wito kuadhimisha miaka 50 ya Jumuiya Zetu Tanzania.**

# Tafakari: MAADHIMISHO YA SIKU YA VIJANA DUNIANI YAACHA NURU

## Papa Akutana na Vijana Duniani

**Kumbukumbu ya Bikira Maria alipowatokea Watoto watatu wa Fatima: Francis, Yacinta Marto na Lucia dos Santos, Mei 13 1917. Ni chanzo cha Maadhimisho ya Siku ya 37 ya Vijana Ulimwenguni 2023: Bikira Maria wa Fatima, Ureno.**

Baba Mtakatifu Francisko kuanzia Agosti 2, 2023 alishiriki maadhimisho ya Siku ya 37 ya Vijana Ulimwenguni. Hii ni hija yake ya 42 ya Kitume Kimataifa na mwendelezo wa tema kuhusu dhamana na utume wa Bikira Maria katika maisha ya Kanisa. Papa alipata nafasi ya kutembelea Madhabahu ya Bikira Maria wa Fatima, nchini Ureno Jumamosi Agosti 5, 2023



Kumbukumbu ya Bikira Maria alipowatokea Watoto watatu wa Fatima: Francis, Yacinta Marto na Lucia dos Santos, Mei 13 1917

2023. Aliongoza Ibada ya Rozari Takatifu kwa vijana wagonjwa: Muhimu akisisitiza Utakatifu, toba na wongofu! **Na Padre Richard A. Mjigwa, C.PP.S.- Vatican**.

Awali, Baba Mtakatifu Francisko katika ujumbe wake kwa njia ya mitandao ya kijamii, aliwaalika vijana kabla ya kuanza safari ya kushiriki maadhimisho ya Siku ya 37 ya Vijana Ulimwenguni, Jimbo kuu la Lisbon, nchini Ureno au katika nchi zao, kufanya tendo la huruma kwa kuwatembelea wazee wanaoishi peke yao. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, sala na maombi ya wazee yatawalinda na kuwajalia kubeba nyoyoni mwao baraka za wazee! Maadhimisho ya Siku ya Vijana Ulimwenguni kwa Mwaka 2023 yalifunguliwa rasmi kwa Ibada ya Misa takatifu Agosti 1- 6, 2023, kwa kunogeshwa na kauli mbiu "***Maria aliondoka akaenda kwa haraka***." Lk. 1:39.

Mwenyezi Mungu kwa njia ya mahusiano na mafungamano kati ya vijana wa kizazi kipya na wazee, wanatambua kwamba, wameitwa

kukuza na kudumisha kumbukumbu na kutambua uzuri wa kuwa ni sehemu ya historia kubwa zaidi. Baba Mtakatifu anaweka mkazo akisema, urafiki na wazee unaweza kuwasaidia vijana kuona maisha yao si tu kwamba, ni jambo la mpito na kwamba, si kila kitu kinawategemea wao na uwezo wao.

Kwa wazee, uwepo wa kijana katika maisha yao unaweza kuwapa matumaini kwamba, uzoefu wao hautapotea bure na kwamba, ndoto zao zinaweza kupata utimilifu katika maisha ya vijana wa kizazi kipya.

Baba Mtakatifu Francisko wakati wa Sala ya Malaika wa Bwana, kwenye Uwanja wa Kanisa kuu la Mtakatifu Petro mjini Vatican, Dominika ya Julai 30, 2023 aliwaalika waamini pamoja na watu wote wenye mapenzi mema, kumsindikiza katika Maadhimisho ya Siku ya 37 ya Vijana Ulimwenguni, fursa ya vijana kukutana na Kristo Yesu pamoja na ndugu zao katika Kristo, huku wakiongozwa na Bikira Maria ambaye baada ya kupashwa habari kwamba, atakuwa ni Mama wa Mungu aliondoka akaenda kwa haraka.

Bikira Maria ni nyota angavu ya safari ya Kikristo anayeheshimiwa sana nchini Ureno! Baba Mtakatifu amewakabidhi mahujaji wa Maadhimisho ya Siku ya 37 ya Vijana Ulimwenguni pamoja na vijana wenyewe chini ya ulinzi na tunza ya Bikira Maria, Mama wa



Bikira Maria wa Fatima, Faraja kwa walimwengu

Mungu na Kanisa.

Bikira Maria wa Fatima, Faraja kwa walimwengu

Hii ni hija yake ya 42 ya Kitume Kimataifa na mwendelezo wa **tema kuhusu dhamana na utume** wa Bikira Maria katika maisha ya Kanisa. Itakumbukwa kwamba, Maadhimisho ya Siku ya Vijana Ulimwenguni kwa Mwaka 2019 yalifanyika huko Panama, kuanzia Januari 22 – 27, 2019, yakinogeshwa na kauli mbiu "***Mimi ni mtumishi wa Bwana nitendewe kama ulivyonena***" Lk. 1:38.

Katika maadhimisho haya, Mama Kanisa kila mwaka ifikapo Mei 13 anaadhimisha kumbukumbu ya Bikira Maria wa Fatima, ikiwa ni kumbukumbu ya Bikira Maria alipowatokea Watoto watatu wa Fatima: Francis, Yacinta Marto na Lucia dos Santos, Mei 13, 1917 na kujitambulisha kuwa ni Bikira Maria wa Rozari Takatifu, kwa kuwakabidhi watoto hawa ujumbe wa matumaini kwa binadamu wote akiwataka wajizatiti katika kupambana na ubaya, kwa kusimama

kidete kulinda, kutetea na kushuhudia imani kwa Kristo Yesu na Kanisa lake.

Ujumbe wa Bikira Maria kwa Watoto wa Fatima unaweza kufupishwa kwa maneno makuu matatu: Sala, Toba na Wongofu wa ndani! Sala ni majadiliano ya kina kati ya mwamini na Muumba wake; majadiliano yanayomwongoza mwamini kuelekea katika maisha ya uzima wa milele. Waamini wanachangamotishwa na Mama Kanisa kutubu na kumwongokea Mwenyezi Mungu kwa kuwa na mwelekeo mpya katika maisha yao. Bikira Maria wa Fatima anawaalika waamini ***kuchuchumilia*** utakatifu na kuendelea kusali kwa ajili ya toba na wongofu wa ndani; kwa kujiweka wakfu kwa Moyo wake usiokuwa na doa!



Bikira Maria wa Fatima, Nyota ya Uinjilishaji Mpya

**Bikira Maria anawaalika waamini kusali Rozari Takatifu ili kuombea amani duniani!**

**Hii ni chngamoto endelevu hata kwa watu wanaoishi katika ulimwengu mamboleo!**

Ujumbe wa Bikira Maria kwa Watoto wa Fatima ***unafumbatwa*** kwa kiasi kikubwa katika Injili, kiasi kwamba, Fatima inakuwa ni shule ya imani na ushuhuda wa maisha ya Kikristo, na Bikira Maria ndiye Mwalimu wake mkuu! Bikira Maria anawaalika waamini pamoja na watu wote wenye mapenzi mema kuwa na imani kwa Kristo Yesu na kamwe wasikatishwe tamaa na: Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia; majanga katika maisha ya watu; tawala za kifashisti na kikomunisti, tawala ambazo zimedhalilisha haki msingi, utu na heshima ya binadamu; kiasi hata cha kutaka kumng'oa Mungu katika maisha na vipaumbele vya mwanadamu. Kilio cha waamini kilikuwa ni kumwomba Mwenyezi Mungu asimame mwenyewe na kujitetea!

Ujumbe wa Bikira Maria kwa Watoto wa Fatima ulijikita zaidi katika Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia na Vita Kuu ya Pili ya Dunia; vita ambavyo vilisababisha madhara makubwa kwa maisha ya watu sehemu mbalimbali za dunia. Siri zote za Bikira Maria kwa Watoto wa Fatima zikafunuliwa hadharani kunako Mwaka 2000 kwa kuonesha madhara makubwa yaliyosababishwa na Urusi kwa wakati ule kwa kupandikiza "ndago" za Ukanimungu; dhuluma, nyanyaso na mauaji ya kikatili dhidi ya Wakristo!

Katika kipindi hiki cha utawala wa giza na chuki dhidi ya imani ya Kikristo, hapa kukaibuka makundi ya Wakristo waliosimama imara kutangaza na kushuhudia imani yao kwa Kristo Yesu, aliyeteswa, akafa na kufufuka kwa wafu! Jeuri ya maisha yao ya kiroho! Mtakatifu Yohane Paulo II, kunako Mei 13, 1981 akiwa kwenye Uwanja wa Kanisa Kuu la Mtakatifu Petro mjini Vatican akapigwa risasi katika jaribio la kutaka kumuua na kumfutilia mbali kutoka katika historia na uso wa dunia! Lakini akasalimika na kwamba, huu ni muujiza wa pekee kabisa aliotendewa na Bikira Maria wa Fatima. Mtakatifu Yohane Paulo II akaamuru hata ile Siri ya Tatu ya Fatima iwekwe hadharani!

Ni siri ambayo ilionesha kwamba kulikuwa na mapambano makali dhidi ya Kanisa.

Mtakatifu Yohane Paulo II akachukua risasi iliyotoka mwilini mwake na kuiweka kwenye taji ya nyota kumi na mbili zinazopamba kichwa cha Bikira Maria wa Fatima.



Maadhimisho ya Siku ya 37 ya Vijana Ulimwenguni 2023.

**Machi 25, 1984 Mtakatifu Yohane Paulo II akauweka ulimwengu na kwa namna ya pekee kabisa, Urussi chini ya ulinzi na tunza ya Moyo Safi wa Bikira Maria.**

Ujumbe wa Bikira Maria kwa Watoto wa Fatima ni endelevu hata kwa watu wa nyakati hizi kwani unafumbatwa katika Injili ya Kristo na Kanisa lake; Unahimiza Ibada kwa Bikira Maria, Toba, Wongofu wa ndani,

Utakatifu wa maisha na umuhimu wa kusali Rozari Takatifu ili kuombea amani duniani. Waamini watambue daima kwamba, hata katika shida na mahangaiko yao, Mwenyezi Mungu daima yuko pamoja nao hadi utimilifu wa ***dahari!*** Bikira Maria anataka kuwaachia watoto wake, ujumbe wa matumaini, wokovu, amani na kwamba, Mwenyezi Mungu apewe kipaumbele cha kwanza katika maisha ya mwanadamu!

"***Maria aliondoka akaenda kwa haraka***." Lk. 1:39 ni kauli mbiu iliyochambuliwa na Makardinali 20 wakisaidiana na Maaskofu 700 walioshiriki katika maadhimisho ya Siku ya Vijana Ulimwenguni wakiwemo zaidi ya mapadre 10,000 na vijana milioni moja na nusu.

# Tafakari: MAADHIMISHO YA SIKU YA VIJANA ULIMWENGUNI YAACHA TAATHIRA

Bikira Maria alipoambiwa kwamba, angekuwa ni Mama wa Mungu hakukaa kitako na kuanza kujipiga picha, bali aliondoka kwa haraka, akaenda hata nchi za milimani, ili kuhudumia na kumsaidia binamu yake Elizabeti aliyekuwa mjamzito!

Huu ni mwaliko kwa vijana kujifunza kutoka kwa Bikira Maria, ili kuondoka kwa haraka kwa ajili ya kuwasaidia wengine. Baba Mtakatifu Francisko anasema, Jimbo kuu la Lisbon, Ureno limechaguliwa kuwa mwenyeji wa Maadhimisho ya Siku ya 37 ya Vijana Ulimwenguni, ili kupandikiza mbegu ya matumaini kwa siku za usoni; mahali ambapo upendo unapewa kipaumbele cha kwanza.

**Maadhimisho ya Siku ya 37 ya Vijana Ulimwenguni iwe ni fursa ya kupandikiza mbegu ya matumaini na kuhakikisha kwamba, upendo unapewa kipaumbele katika maisha. Maadhimisho hayo yalitimua vumbi huko Jimbo Kuu la Lisbon, Ureno kuanzia Agosti 1 – 6, 2013 yakinogeshwa na kauli mbiu: "Maria aliondoka akaenda kwa haraka." (Lk. 1:39).**

Jumuiya ya Kimataifa inashuhudia vita na mipasuko ya kijamii sehemu mbalimbali za dunia na kwamba, watu wanahitaji ulimwengu mpya ambao hauogopi kutangaza na kushuhudia tunu msingi za Kiinjili, kuwatangazia watu wa Mataifa ile furaha ya Injili.

Baba Mtakatifu Francisko anawaalika vijana wa kizazi kipya kusali ili kwamba, Maadhimisho ya Siku ya 37 ya Vijana Ulimwenguni yawasaidie vijana wa kizazi kipya kujielekeza zaidi katika kutangaza na kushuhudia tunu msingi za Kiinjili katika uhalisia wa maisha yao.

Nia za Baba Mtakatifu Francisko zinasambazwa sehemu mbalimbali za dunia kwa njia ya Mtandao wa Sala Kimataifa ambao umeundwa kwa kushirikiana na Mfuko wa Maadhimisho ya Siku ya Vijana Ulimwenguni, Lisbon 2023, Baraza la Kipapa la Walei, Familia na Maisha kwa ajili ya vijana wa kizazi kipya. Baba Mtakatifu anawaalika vijana kujizatiti kwa haraka kutangaza na kushuhudia Habari Njema ya Wokovu.

Baba Mtakatifu katika ujumbe wake, anajitahidi kujibu maswali ya msingi yaliyoulizwa na vijana wa kizazi kipya kutoka nchini Ufilippini, Brazil na Pwani ya Pembe, ambao ni umoja wa wanachama wa Harakati za Vijana wa Kiekaristi "Eucharistic Youth Movement, EYM" unaoundwa na vijana 1, 700, 000 kutoka katika nchi 60 duniani. Hawa wanamuuliza Baba Mtakatifu kwa nini kama Kanisa ni kwa ajili ya wazee peke yao na kwa nini aliamua kuchagua tema ya Bikira Maria ili kunogesha maadhimisho haya.

Akijibu hoja hiyo, Kardinali mteule Américo Manuel Alves Aguiar, Rais wa Mfuko wa Maadhimisho ya Siku ya Vijana Ulimwenguni, Lisbon kwa Mwaka 2023 ambaye pia ni Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Lisbon, nchini Ureno anasema, Kanisa linawahitaji vijana wa kizazi kipya ili liendelee kuwa kijana, hili ni tukio la vijana wanaokutana na Baba Mtakatifu Francisko; ni tukio linalowakutanisha vijana kutoka sehemu mbalimbali za dunia, ni tukio linalowakutanisha vijana na Kristo Yesu aliye hai.

Kwa hakika, vijana wengi wataguswa na maneno ya Baba Mtakatifu Francisko katika maadhimisho haya, kwa kutambua kwamba, vijana kimsingi wanakutana na Kristo Yesu kila siku ya maisha yao, changamoto na mwaliko wa kujisadaka bila ya kujibakiza sanjari na kujiaminisha mbele ya Mwenyezi Mungu na kwa Kristo Mfufuka.

Naye Padre Joào Chagas, Mkurugenzi wa Idara ya Vijana, Baraza la Kipapa la Walei, Familia na Maisha anasema, inapendeza kwa vijana kusali, kutafakari sanjari na kujadiliana, kwani vijana wanazo ndoto, lakini wanahitaji hekima, busara na maono ya wazee. Vijana wanaweza kuruka na kupaa, lakini wanahitaji kugundua mizizi na asili yao, yaani kutambua historia ya maisha yao. Ndiyo maana kuna haja ya kujenga na kudumisha utamaduni wa watu kukutana na hasa baada ya maambukizi makubwa ya Ugonjwa wa Virusi vya Korona, UVIKO-19, uliopelekea watu kujitenga.

# Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo(JNNK) katika Jimbo la Musoma na Nchi za AMECEA (Afrika Mashariki na Kati).

**Toleo lililopita tuliahidi kuja na Historia Fupi ya Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo**

## Mambo Yalianza Hapa

Inawezekana hakuna kumbukumbu za kihistoria za kutosha zilizohifadiwa katika makavasha ya Jimbo la Musoma zinazodhihirisha **Mambo Yalianza Hapa**. Wengine waliotunza kumbukumbu zao wanataja Jamhuri ya Kongo (DRC). Wanadhania tu, kuwa huko zipo kumbukumbu za maandishi hasa baada ya Mkutano Mkuu wa Baraza la Maaskofu wa Nchi ya Jamhuri ya Kongo wa Novemba 20 – Desemba 2, 1961 uliopitisha mpango wa kichungaji wa kuhamasisha Jumuiya hai za Kanisa ambazo wakati mwingine ziliitwa Jumuiya hai za Kikristo (Kiongozi, Agost 11-17, 2023).

Sehemu kubwa ya Kongo na nchi za Afrika Mashariki ziliongozwa na wamisionari kutoka Ufaransa na wengi walikuwa Wamisionari wa Afrika au White Fathers. Kwenye majimbo yote waliweka mpango wa kuhamasisha Jumuiya za Kikristo kama kipaumbele cha kuanzisha na kueneza jumuiya za Kikristo ili kusaidia

na kuliwezesha Kanisa kuwa la Kiafrika na kuwa karibu zaidi na watu. Huo ni ukweli kutoka falsafa ya Mwasisi wa Shirika hilo Mwadhama Charles Kardinali Lavigerie wa Algiers.

Hapo Nyegina Wamisionari wa Afrika walijenga makambi ya waamini yaliyotengwa katika Jumuiya ndogo ndogo za Kikristo kwa kuzingatia makabila yao.

Hawa walikuwa na sababu za msingi kutokana na changamoto ya lugha. Kila jamii ilielekezwa eneo lake tangu awali. Waliishi katika kambi hizo na kushirikiana kulima bega kwa bega na kushirikiana kazi zote wakati wakiendelea na mafunzo ya katekesi, wakijifunza ukatekumeni na kipaimara kwa lugha ya Kikwaya hata kabla na baada ya kusimikwa Parokia ya kwanza ya Nyegina mwaka 1911. Waliohitimu mafunzo ya msingi ya dini waliwasha mshumaa na kuondoka kurudi maeneo ya jamii zao kuanzisha Jumuiya mpya na vigango vilivyostawi haraka na kupandishwa hadhi kuwa Parokia. Wengine walifurahia maisha ya Ukristo na kujenga makazi ya kudumu hapo Nyegina wakiunganishwa kupitia vyama vya kitume hasa Legio Maria, Moyo Mtakatifu wa Yesu na vingine.

Jitihada za awali za kujengeka Jumuiya hai zilizosisimua, zilizoishi Kikristo kwa mfano wa historia tunayosoma katika Matendo ya Mitume ziliibuka kwenye Parokia tano za jamii ya Waluo (Nyarombo, Kowak, Masonga, Ingri na Tatwe).

**JUMUIYA NDOGO NDOGO ZA KIKRISTO (JNNK)**

Miongoni mwa mambo yaliyotukuza Jimbo la Musoma ni chimbuko la historia ya ujenzi wa Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo (JNNK) katika Afrika Mashariki. Msichana wa Kifaransa, jina lake Marie France Perrin alisafiri kutoka Bara la Ulaya hadi Musoma. Alifika jimboni humo mwaka 1965 akiwa na lengo la kufanya utafiti kuhusu Jumuiya za Kikristo katika madhehebu ya Kikristo yaliyoanzishwa na Waafrika wenyewe.

Utafiti wake aliuendesha katika Jamii ya Waluo wa Wilaya ya Rorya (Wakati huo North Mara na baadaye Tarime). Mtafiti huyo, Marie France Perrin aliweka vituo katika Parokia za Ingri, Masonga, Kowak na Nyarombo; maeneo ambayo yalikuwa chimbuko la madhehebu mapya ya Kikristo yasiyopungua 20 yaliyoanzishwa na wazalendo.

Mengine yaliibuka kutoka nchi jirani ya Kenya lakini mengi yalianzia Tanzania kuelekea huko nchi jirani.

Chanzo cha uchunguzi wake ni matokeo ya kazi za Kimisionari za Wamisionari kutoka Ufaransa alizosoma kwenye majarida ya Kifaransa. Hata hivyo eneo lililopokea haraka wito wa kuunda jumuiya za awamu ya pili chini ya Shirika la Maryknoll ni Parokia ya Nyarombo mwaka 1959.

Baada ya kuchapisha matokeo ya uchunguzi wa awali, mapadre Daniel Zwack na Gerard Pavis wa Maryknoll waliokuwa wanafanyakazi ya utume hapo Nyarombo walivutiwa na mwenendo wa

madhehebu ya Kikristo. Wakati fulani mapadre hao waliweza kuandamana na mtafiti huyo, wakachochewa na maisha ya jumuiya hizo za madhehebu mapya hasa walipoona jinsi jumuiya zao zilivyojiongoza zenyewe kwa kujitungia sala, nyimbo, na kuchapa kazi za mikono na zaidi kuhudumiana katika shida na raha.

**Matokeo ya Utafiti**:

Katika Kitabu cha Mambo Yalianza Hapa na Safari ya Imani, 1985-2022), Mwandishi na Mtafiti wa Jumuiya za Kikristo Daniel Msangya amebainisha dhahiri mashujaa wa Jumuiya za Kikristo waliovutia hisia za maaskofu wa AMECEA. Ndipo mapadre hao wakaanza kuhimiza wakristo wa Parokia ya Nyarombo waanze kuiga mfano wa madhehebu hayo katika kujitungia sala, nyimbo na kazi za kuhudumiana katika shida.

Wito huo ulizaa matunda. Ulipokelewa kwa mikono yote na kutekelezwa kwa vitendo. Wakristo Wakatoliki wakakubali kwa ari na kuanza kuita Jumuiya zao kwa jina la *Oganda Johera, yaani* Jumuiya za Mapendo.

Jumuiya hizo za awali zilivuma na kuendeshwa kwa nguvu moja na mwamko mpya. Padre Daniel Zwack alikishirikiana na Katekista John Omole. Walianza kueneza mafundisho ya kuishi kijumuiya na kusaidiana. Walipita parokia zote za jamii ya Waluo huko Kowak, Ingri, Tatwe na Masonga wakiungwa mkono na Askofu John Rudin wa Jimbo
la Musoma aliyefurahishwa na mwamko huo mpya wa kukoleza mafundisho ya Injili kwa vitendo.

Watu walishangazwa na mafundisho hayo, wakahamasika kwa wingi wakivutwa na maisha ya Wakatoliki hawa walioacha majukumu mengine kumtumikia Mungu kwa pamoja.

Sifa zao zikavuma Jimboni kote na baadhi ya parokia ziliomba na kupewa fursa ya kupata mafundisho hayo, zilizoweza zilituma waamini wake kushuhudia. Mafundisho hayo yalivuma na kuvuka mipaka ya jimbo. Wakristo wa Parokia hizo tano wakaandika historia ambayo haiwezi kufutika. Nayo imehifadhiwa sasa katika maandishi kitabu.

**Jumuiya ya Mkamilishano**:

Hazikupita siku nyingi cheche za moto wa Jumuiya zikaanza kusambaa. Habari zikasikika kutoka majimbo mengine. Jimbo la Rulenge lilitangulia kupokea taarifa hizo. Askofu Christopher Mwoleka alizipata awali kupitia kwa Askofu Lanctot Mmisionari wa White Fathers. Alikuwa na taarifa za Jimbo la Musoma zilizopata kuvuma.

Alivutiwa na kuonyesha haraka nia ya kueneza maisha haya. Hakupoteza muda. Alifunga safari yeye mwenyewe akiwa na mapadre wake wawili. Alitembelea Parokia ya Nyarombo ili kujionea na kujifunza mwenyewe. Askofu Mwoleka pia alipitia parokia nyingine za Tatwe, Masonga, Kowak na Ingri. Akashuhudia maisha ya jamii za Waluo waliokuwa wamepiga hatua wakiishi katika Jumuiya za upendo (*Oganda Johera*). Alipata ushahidi na uhakika wa mambo aliyoyaona kule Nyarombo.

Baada ya kujifunza kwa muda wa wiki moja zaidi, aliongoza msafara wake kurudi jimboni mwake na kuanzisha jumuiya zake zilizoishi maisha ya Ukristo. Akaziita Jumuiya za *mkamilishano*.

Mwaka 1993 mwandishi wa makala haya akiwa na Padre Joseph Healey, MM walitembelea Jumuiya hizo huko Parokia za Buhororo, Karagwe, Bushangaro, Bugene na Isingiro kushuhudia Jumuiya zilizoendeshwa kwa kufuata maisha ya Ujamaa na Kujitegemea. Jumuiya hizo zilichukuwa mfumo wa awali wa Jumuiya za Nyegina zilizoundwa katika makambi ya pamoja au kijiji maalum. Hata Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kuzitembelea Jumuiya hizo.

Hapo palikamilika na wanajumuiya walikamilishana kwa mapaji na karama. Kulikuwa na mapadre, mabruda na masista, kulikuwa na walei, na wote wakiwa wamoja, wakiishi kwa usawa na kushirikiana maisha na vipaji. Walifanya kazi kama mchwa, wakishirikiana na kusali pamoja, wakilima pamoja walikula pamoja, walishona, wakafuma, walichonga, walijenga, walisali pamoja asubuhi, mchana na jioni na kulima kwa kufuata misingi ya kitaalam kwa kutumia teknolojia.

Miradi ya yao ya maendeleo ilikuwa ya kisasa zaidi na Askofu Mwoleka alihangaika duniani kote kutafuta uwezeshwaji kifedha, kitaalamu, kiufundi na vitendea kazi. Walifikia hatua ya kusomesha watoto na vijana wakilipia mahitaji ya shule katika ngazi zote ndani na nje ya jimbo hilo.

"*Wanaishi pamoja, kwa umoja; kwa shida na raha; kwa kazi na huduma. Wanakula pamoja na kuimba pamoja…ndiyo maisha ya Jumuiya ya Mkamilishano iliyoishi Ukristo kwa vitendo*," nukuu ya Askofu Mwoleka, kama ilivyoandikwa na Daniel Benno Msangya katika makala ya Jarida la ***New People***, 1993 alipozuru Jimbo la Rulenge akiwa na Padre Joseph Healey, mmisionari na mwanajuiya mwandamizi kutoka Marekani.


Mwanzoni mwa miaka ya 1970 Askofu Mwoleka mwenyewe alijiunga na jumuiya hizo vijijini. Aliaga ofisini. Akaenda kuishi kama mkulima, mwana ujamaa, akabeba jembe na kupalilia mashamba, akasali pamoja na waamini wake na kuwabariki. (*Ref. New People, Msangya, 1993*). Naye Padre Joseph Healey aliandika Kitabu, *The Fifth Gospel*, Injili ya Tano, 1981) akaeleza maisha ya Askofu Mwoleka alivyoishi mashambani na waamini wake katika maisha duni ya utamaduni ndani ya Jumuiya ndogo ndogo za Kikristo.

Askofu Mwoleka alipoona ustawi mzuri wa Jumuiya hizi akaanza kueneza kwa nguvu mafundisho haya kwa maaskofu wenzake nchini Tanzania na kote katika Afrika Mashariki na kusafiri akihudhuria matamasha na makongamano ya kimataifa na kutoa mihadhara. Alianzisha matawi hasa Morogoro na Dar Es Salaam na kuvutia waamini kutoka majimbo mbalimbali kutembelea jumuiya hizo na wengine kujiunga nazo.

**Ngoma ikilia sana kuna lele au hupasuka?**

Hapo penye chimbuko la jumuiya hizo (Parokia ya Nyarombo) mambo yalikwenda mrama.

Hayakwenda sawa. Kulitokea uvumi kuwa watu wasiopenda jumuiya hizo, wenye hinda na hila waliwashitaki mapadre Zwack na Pavis kuwa walinuia kuanzisha madhehebu tofauti na Wakatoliki. Hofu yao ilishinda kwa muda. Kanisa lilikuwa halijajiandaa kupokea ibada za "kilokole" ambazo leo zinaenea kwa kivuli cha ibada za karismatiki (charismatic) zikifuata liturjia ngeni ndani ya Ukatoliki. Kwa mfano wa maombi yenye makelele mengi, yenye imani za kuponya wagonjwa na kufanya miujiza hadharani.




**Askofu Afuta Jumuiya**:

Askofu John Rudin alishituka na kukaa kimya kwa muda akifanya utafiti. Lakini msisitizo ulipomkera masikioni aliamua kupunguza kasi ya Jumuiya za Mapendo.

Jambo hilo liliwahuzunisha mapadre hao Daniel Zwack na Gerard Pavis, ikawapasa kuhama kutoka Nyarombo na kurudi kwao Marekani. Furaha walizokuwa nazo waamini wao zikafifia polepole na kupotea kama moshi unaopepea angani. Padre Daniel Zwack aliporejea Tanzania alihamia Jimbo la Shinyanga. Hakuna simulizi ikiwa aliendeleza Jumuiya lakini yasimuliwa aliporudi Marekani aliingia maisha ya ndoa na kuacha upadre.

## MWANAJUMUIYA WA AFRIKA

Hata hivyo parokia nyingine ziliendeleza jumuiya zao kwa kuungwa mkono na mapadre wao bila Askofu kuzifuatilia.

Mapadre walioonja mafundisho ya maisha ya Kikristo katika Jumuiya Ndogo Ndogo hawakuona sababu za msingi za kufuta kabisa mwenendo wa Jumuiya za mapendo. Padre William Daley na Padre William Sweeney hapo Ingri na Kowak walitia fora. Naye Padre Mike Kirwen aliyekuja Parokia ya Ingri alisukuma kwa nguvu na kuunga mkono Jumuiya alizokuta zimeanza kufifia katika vijiji vya Ingri, Nyambogo, Randa, Ryagoro na Masara. Akazitembelea na kuwatia shime huku akila chochote alichokuta kinaliwa na wanajumuiya.

Akifuatisha mfumo wa jumuiya za awali za Parokia za Jamii za Waluo alisimamia utaratibu wa kuweka viongozi wa kila jumuiya. Na huyo alikuwa Professa aliyefanya tafiti zilizotumika AMECEA. Alitumwa na Shirika lake kuendeleza utafiti. Alijaribisha miongozo ya awali na baadaye

kuwasilisha mapendekezo yake Maryknoll, TEC na AMECEA. Hatuwezi kubainisha mchango wake ulipokelewa vipi na ulisaidia vipi kuunda sera ya Jumuiya kwa sababu Askofu Blomjous wa Mwanza alikuwa amewasilisha tafiti nyingi juu ya maisha ya Mkristo Mwafrika na kuanzisha vituo vya kuendeleza utamaduni na utamadunisho.

Hata hivyo AMECEA walitoa tamko linalotumika kuongoza Jumuiya na huo ukawa mwanzo wa Jumuiya zinazovuma leo Tanzania na nchi majirani.

Taratibu hizo zinatoa fursa ya kuunda Jumuia na kuchagua Mwenyekiti, makamu wake, Katibu, mtunza hazina na viongozi wa ndoa, wasomaji na waongoza Biblia, viongozi wa vijana, na walezi wa wagonjwa na mabalozi.

Zilifanyika semina kila mwezi kuhusu uimarishaji wa jumuiya ndogo ndogo za Kikristo.

Baadhi ya semina zilifanyika Makoko Senta, huku Padre Kirwen (Profesa) akabeba dhamana ya kuwasafirisha waamini na hasa viongozi waliochaguliwa kwenye jumuiya hizo na familia zao hadi Makoko, Musoma.

Yeye mwenyewe alishiriki kutoa mafunzo akisaidiwa na Padre Joseph Masatu, Padre Daudi, Padre John Casey na masista Patricia Titus, Katekista Linus Muga na wengine.

**Maaskofu Wasisitiza Jumuiya**:

Askofu John Rudin alipata taarifa ya maendeleo ya Jumuiya ndogo ndogo za Kikristo kutoka Jimbo la Rulenge. Alishangaa kusikia ripoti nzuri za Askofu Christopher Mwoleka alizotoa kwenye mikutano ya urika wa maaskofu kila walipokutana kwenye Baraza lao la Maaskofu huko Kurasini, Dar es Salaam. Aliziita jumuiya za mkamilishano. Askofu Rudin akavutiwa tena.

Akaanza upya kuhimiza zienezwe kote jimboni Musoma. Padre Alphonse Timira aliteuliwa kueneza habari za Jumuiya Ndogo ndogo jimboni kote hasa katika parokia ambazo hazijaanza kujenga jumuiya hizo. Semina nyingi ziliandaliwa na kuendeshwa hapo Makoko Senta.

Mapadre Mike Kirwen, John Casey, Joseph Masatu, Francis Flynn na Charles Masaga walihusishwa kuwezesha na kuelimisha viongozi wa parokia waliotakiwa kurudi kusaidia kuunda jumuiya hizo. Walielimishwa ubora wa kujenga jumuiya ndogo ndogo na mfumo mpya wa jumuiya uliokuwa umepitishwa na Baraza la Maaskofu Tanzania TEC na AMECEA.

Kitaifa, chachu ya kueneza Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo ilikuwa imeanza kote na kutengeneza wimbi lisilozuilika.

Ubora wa Jumuiya hizo ulianza kueleweka na kuonekana hasa kwa mfano wa Jimbo la Rulenge ambako Askofu Christopher Mwoleka alivuka viwango. Aliwavuta mapadre, masista na mabruda kuishi vijijini na kufanya kazi na jumuiya. Hata hivyo, siyo wote walimuunga mkono. Wengine walipata shida hasa mapadre wachache waliokosoa mwelekeo wake.

Hali kadhalika mafundisho ya jumuiya hizo yaliingizwa katika mwongozo wa Baraza la Maaskofu wa Tanzania (TEC) na Baraza la Maaskofu wa Afrika Mashariki na Kati (AMECEA) na mkazo uliwekwa kuwa jumuiya hizi zijengwe kila mahali.

Jimboni Musoma (zilikoanzia na siyo Kongo) kila parokia ilikuwa imeanzisha jumuiya hizo hadi mwaka 1985. Shirika la Maryknoll lilimteua Padre Joseph Healey kuimarisha jumuiya hizo. Kwa uzoefu alioupata katika Jimbo la Rulenge alikowahi kuishi na Askofu Mwoleka vijijini, wakaishi kijumuiya kwa miaka kadhaa. Hata hivyo, mkazo haukuwekwa kama hapo mwanzo, kama ilivyokuwa katika Jumuiya za Mapendo. Baada ya kuwekewa msisitizo na Baraza la Maaskofu Tanzania, hivi sasa jumuiya za Kikristo siyo jambo geni au la hiari. Imekuwa sehemu ya maisha ya Kikristo.

Padre Joseph Healey alitumia uzoefu wake huko Rulenge na Iramba, akabaki mwanajumuiya imara wa Jumuiya ya Mtakatifu Anna, iliyomlea Padre Biseko (mdogo) katika eneo la Mwisenge.

Walikutana kila Ahamisi wakasali, wakasoma Biblia na kujadili matendo mema. Wakakusanya michango kwa ajili ya kutoa msaada kwa wagonjwa na watu maskini. Mtazamo wao ulikoma katika matendo ya Kikristo kwa faida ya Jumuiya tofauti na mambo yanavyokwenda leo. Jumuiya ni tegemeo la maendeleo ya kanisa katika ngazi zote.

Kimsingi jumuiya za sasa ni hai, ni umoja na mapendo kamili. Padre Healey alipeleka chachu ya jumuiya za Kikristo huko Nairobi. Bado yupo na wanajumuiya wake kiroho na kwa mawasiliano licha ya kuhama na kurudi kwao Marekani. Na Jumuiya aliyojiunga nayo imezalisha Padre wa Kwanza Mwafrika kujiunga na Shirika la Maryknoll baada ya kufungua njia kwa mataifa ya Afrika. Alianza Sr. Efraim Nyaki (1992). Akatumwa Amerika Kusini. Leo Maryknoll imevaa nguo mpya.

Waamini wanashirikiana kwa matumaini na kanisa linaamini kuwa maisha haya ndiyo matumaini yake kwa siku zijazo katika Kanisa la Afrika Mashariki na kote duniani. **Leo tutafikia hapa na katika toleousikose mwendelezo wa makala haya yakimulika mwongozo wa AMECEA na Tamko Rasmi la Maaskofu wetu kupitia Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania, TEC hasa juu ya maandalizi ya maadhimisho ya miaka 50 ya Jumuiya za Ndogo Ndogo Kikristo katika ngazi mbalimbali.**

**Kwa ajili ya Mateso yake Makali: Utuhurumie Sisi na Dunia Nzima**

**Mungu Mtakatifu, Mtakatifu mwenye Enzi, Mtakatifu Usiyeweza Kufa**

**Utuhurumie Sisi na Dunia Nzima**




**TUNAWAALIKA WAJUMBE/KIONGOZI WA KAMATI YA MAADHIMISHO YA JUBILEI YA MIAKA 50 YA JNNK JIMBO LA MUSOMA KUJA NA TAMKO LA JIMBO AU BARAZA LA MAASKOFU TANZANIA(TEC)NA KUWAPA WASOMAJI WETU TAARIFA YA MAANDALIZI HAYA. JE, JIMBO LA MUSOMA LIMEJIANDAA VIPI?**

# MAKALA ZA ROHONI MWEZI WA ROZARI

## HISTORIA FUPI YA ROZARI TAKATIFU

**Utangulizi**

Kila mwezi Oktoba waamini Wakatoliki wanaalikwa kusali Rozari kwa mwezi mzima. Lengo kubwa ni kumweshimu na kumshukuru Mama Bikira Maria, Mama wa Mungu kwa maombezi yake ya kimama kwetu sisi wanadamu.



**Katika makala haya *Daniel Benno Msangya* anakumbushia wito wa Mama Kanisa kwa Mwezi wa kumi kila mwaka kuwa ni fursa nyingine tena ya kumwendea Mama Bikira Maria na kumshirikisha furaha, shukrani, taabu, changamoto na matarajio yetu kwa njia ya Rozari Takatifu ambayo hutupa nafasi ya kutafakari mafumbo ya maisha ya Yesu na Maria katika safari ya wokovu wetu. Hivyo tukiwa kwenye Mwezi wa Rozari tunatumia fursa hii kudadavua ukwasi wa Rozari, tunu, manufaa na amali zilizomo na kupitia walau kwa ufupi historia ya Rozari Takatifu.**

1. **Dhana na Dhima**: Rozari ni sala nzuri yenye utajiri wa neema, na sala inayogusa kwa karibu Moyo Safi wa Mama wa Mungu. Ni sala yenye ahadi inayothibitishwa na kanisa. "…Ikiwa unataka amani itawale katika nyumba zenu, salini Rozari katika familia." (**Baba Mtakatifu Mt. Pius X**)

**2. Asili ya neno "Rozari"**

Neno la Kiingereza "rosary" linatokana na neno la Kilatini "Rozarium" lenye maana ya "bustani ya mawaridi" (rose garden) au "taji la mawaridi". Kwa kadiri ya desturi ya watu wa Ulaya kupeana maua ya mawaridi ni moja ya matendo yenye lengo la kuonesha upendo wa hali ya juu kwa mtu Fulani, hasa wakati wa furaha au huzuni; mawaridi pia ni zawadi kubwa ya upendo hasa baina ya wapenzi. Sisi Wakristo Mama Bikira Maria ni mpenzi wetu na zawadi kubwa tunayoweza kumpa ni "kusali rozari" ambayo ndiyo "mawaridi yetu kwake". Kwa kadiri ya mapokeo mawaridi, hasa meupe yanamwakilisha Bikira Maria asiye na doa, yaani ni mweupe kama waridi jeupe.

3. **Historia ya awali ya Rozari**

Katika zama za kwanza za Ukristo (karne ya 3 na ya 4) walikuwepo Wamonaki (*monks)* na Wahermiti ambao waliamua kuishi injili kwa ukamilifu na hivyo kuamua kuishi maisha ya upweke ama mmoja mmoja au kama kikundi. Wamonaki waliamua kuishi maisha ya pamoja huku lengo lao kuu likiwa kusali na kuishi mashauri ya injili ambayo ni usafi wa moyo, utii na ufukara. Wamonaki kwa kipindi hicho walikuwa ni wasomi ingawa walikuwa wachache. Hivyo waliamua, kama sehemu ya maisha yao ya sala, kusali Zaburi zote 150 kila siku.

Hata hivyo baadaye waliamua kuwa angalau wawe wamesali Zaburi zote 150 kwa wiki. Ili kuweza kuzihesabu wakati wa kusali bila kuchanganya waliamua kukusanya ama changarawe, mbegu ndogo za matunda au kokoto 150 na kila walipomaliza zaburi moja walichukua changarawe, mbegu au kokoto moja na kuitupa kwenye chombo mfano wa debe au ndoo au kikapu au mfuko ili kujua wamefika zaburi ya ngapi. Baadaye, ili kuweza kuhesabu vizuri na kwa urahisi zaidi waliamua kutumia kamba ndefu ambayo waliiwekea vifundo 150 sawa na jumla ya zaburi zote 150.

Watu wa kawaida walioishi jirani na nyumba za wamonaki walitamani sana kujiunga nao na kusali zaburi hizo 150. Kwa bahati mbaya wengi wa watu hao walikuwa hawajui kusoma wala kuandika na hata teknolojia ya uchapaji ilikuwa bado ipo chini sana na hata wengi wao hawakuwa na muda wa kutosha wa kuweza kusali zaburi zote. Hivyo ili kuonesha nia yao ya kusali zaburi 150 pamoja na Wamonaki, majirani hao waliamua kuwa watakuwa wanasali sala ya Baba Yetu mara 150 wakati Wamonaki wanasali zaburi zote 150.

Mwanzoni Wakristo hao wasio Wamonaki waliiga pia namna ya kuzihesabu Baba Yetu kwa kutumia kokoto, mbegu za matunda, mawe au changarawe.

Baadaye walianza kutumia ushanga uliopitishwa kwenye kamba (*string of beads*). Hata sisi leo tunatumia Rozari iliyotengenezwa kwa namna hiyo. Inasemekana kuwa Mt. Peter Damiani mnamo karne ya 11 alitoa ushauri wa kusali Salamu Maria 150 badala ya Baba Yetu 150.

Kumbe tangu hapo Wakristo wakaanza kusali Salamu Maria 150 huku wakiendelea kutumia kamba iliyowekewa mafundo 150 au shanga 150 zilizopitishwa kwenye kamba ili kuwasaidia kusali vizuri. Baadaye mnamo mwaka 1365 Mmonaki

aitwaye Henry wa Kalkari (1328-1408) alizigawa Salamu Maria 150 katika makundi 15 yenye Salamu Maria 10 kila moja. Pia aliweka Baba Yetu kila baada ya Salamu Maria 10. Hivyo sala ya Rozari ikawa na Salamu Maria 10 zinazorudiwa mara 15 zikiambatana na Baba Yetu kila baada ya Salamu Maria 10. Ingawa sisi leo tunatumia Rozari yenye takribani Salamu Maria 50 bado kuna Rozari ambayo ina jumla ya Salamu Maria 150 kwa wakati mmoja.

4. **Mt. Dominiko na historia ya Rozari**

Ingawa Mt. Dominiko yeye mwenyewe hakuwahi kusema au kuandika kuwa ametokewa na Bikira Maria na kupewa Rozari na kufundishwa kuisali ili awafundishe wengine, masimulizi yanamhusisha Mt. Dominiko kama chanzo cha Rozari kama tuijuavyo leo. Mwenyeheri Allan de la Roche katika maandishi yake anadai kuwa alifunuliwa katika ndoto na kumuona Mt. Dominiko akipewa rozari na Bikira Maria. Mbali na Dominiko kutajwa na Mwenyeheri Allan de la Roche, Mababa Watakatifu wengi wamemtaja pia Mt. Dominiko kama mtu anayehusika na asili ya rozari katika mwonekano wa sasa. Inasemekana kuwa wakati huo kulikuwa na kundi la wazushi hasa Ufaransa na Italia waliokuwa wanapita kwa watu na kufundisha mafundisho potofu huku wakikataa fumbo la umwilisho (nafsi ya pili ya Mungu kuchukua mwili na kuwa binadamu), walipinga fundisho la Kanisa juu ya uwepo wa masakramenti na walikuwa wakiyapigia debe matendo ambayo Kanisa lilifundisha kuwa ni maovu.

Mt. Dominiko alipambana nao kwa udi na uvumba lakini juhudi zake hazikuzaa sana matunda. Kwa mujibu wa Mwenyeheri Allan de la Roche, Bikira Maria alimtokea Mt. Dominiko mnamo mwaka 1214 na kumwambia kuwa ili kuwashinda wazushi hao anapaswa kueneza ibada ya rozari na hivyo kumfundisha Mt. Dominiko. Mara baada ya kuanza kuisali na kuwafundisha watu wengine kundi hilo la wazushi lilitokomea kabisa kwani wengi wao waliongoka na kurudia mafundisho ya kweli.

Hivyo, kwa njia ya Rozari Takatifu Kanisa lilipata ushindi dhidi ya wazushi.

Hivyo tokea wakati wa Mt. Dominiko hadi mwaka 1930 Rozari ilikuwa na jumla ya sala tano:

Kanuni ya Imani ya Mitume, Salamu Maria, Atukuzwe Baba, Baba Yetu na Salamu Malkia. Sala hizi hazikuwekwa siku moja tu na kukamilisha Rozari bali zilikuwa zinawekwa katika vipindi tofauti vya historia ya Rozari. Katika tokeo la Bikira Maria kwa watoto watatu (Lucia, Francisco na Jacinta) huko Fatima Ureno mnamo Julai 13, 1917, Bikira Maria aliagiza watoto hao kuongeza maneno "Ee Yesu Mwema, Utusamehe dhambi zetu, Utukinge na moto wa milele, Ongoza roho zote mbinguni, hasa za wale wanaohitaji zaidi huruma yako" kila baada ya Salamu Maria 10. Sala hii inaitwa Sala ya Fatima. Mwaka 1930 Kanisa lilitamka wazi kuwa Sala ya Fatima itumiwe na Wakristo wote wa kanisa zima wasalipo Rozari. Sala hii ilifanya rozari kuwa na jumla ya sala sita (6).

Kuanzia karne ya 16 hadi mwanzoni mwa karne ya 21 kulikuwa na makundi matatu ya mafumbo ya Rozari: Mafumbo ya Furaha, Mafumbo ya Utukufu na Mafumbo ya Uchungu. Mwaka 2001 Baba Mtakatifu Yohane Paulo II aliongeza Mafumbo ya Mwanga. Nia kubwa ilikuwa ni kuwafanya waamini watafakari maisha ya Yesu kati ya kuzaliwa kwake na Mateso yake.

5. **Kwa nini mwezi wa 10 ni mwezi wa Rozari?**

Kanisa limeweka mwezi Mei na Oktoba kuwa miezi ya kumweshimu Mama Bikira Maria. Wengi wetu hufahamu tu mwezi Oktoba. Mwezi Mei ni mwezi wa Bikira Maria kwa kuwa Bikira Maria aliwatokea Lucia, Francisco na Jacinta huko Fatima Ureno kwa mara ya kwanza Mei 13, 1917 ujumbe mkuu ukiwa kuhangaikia wokovu wa roho za binadamu kwa njia ya kusali rozari na ibada kwa Moyo Safi wa Bikira Maria.

Mwezi wa 10 ni mwezi wa kusali Rozari Takatifu. Kuchaguliwa kwa mwezi wa 10 kuna msingi wake katika historia ya Kanisa.

Waislam wa Kituruki miaka ya 1500 waliamua kutumia mwanya wa vuguvugu la kujitenga kwa Waprotestanti kutoka Kanisa Katoliki. Hivyo waliamua kuvamia nchi za Ulaya ili kueneza dini yao kwa nguvu ya upanga na vita kwa kuwalazimisha Wakristo kuwa Waislam.

Oktoba 7, 1571 Waislam wa Kituruki waliamua kuivamia Italy kwa kuanzisha vita ya baharini iliyojulikana kama Vita vya Lepanto (Ugiriki). Baba Mtakatifu wa wakati huo alikuwa Pius V.

Baba Mtakatifu alijua wazi kuwa Waislam walikuwa ni wengi kwa idadi kuliko Wakristo na ya kuwa Waislam walikuwa na meli nyingi za kivita kuliko Wakristo.

Hata hivyo Baba Mtakatifu aliamuru jeshi lake likisaidiwa na wanajeshi kutoka Spain kwenda baharini kupambana na Waislam. Baba Mtakatifu aliamuru kila

askari abebe Rozari na kuisali wanapokuwa vitani majini;



pia aliamuru wananchi wa Italia waliobaki majumbani wafanye maandamo makubwa huku wakisali Rozari kuomba msaada wa Bikira Maria ili Wakristo washinde vita. Yeye mwenyewe alisali Rozari siku hiyo ya Oktoba 7.

Muda si mrefu habari zilimfikia Baba Mtakatifu kuwa Wakristo wameshinda vita na kati ya meli 242 za Waislam zimesalia meli 12 tu huku jumla ya Waislam 30,000 wakiwa wameuwa, takribani 8,000 wamejeruhiwa au kutekwa. Kwa upande wa Wakristo ni watu 7,500 tu waliokuwa ama wameuawa au wamejeruhiwa au kutekwa ambao baadaye wengi wao walifanikiwa kutoroka. Baba Mtakatifu Pius V alitamka kuwa ushindi huo haujatokana na weledi wa askari wala ubora wa vifaa vya kivita bali ni ushindi uliotokana na maombezi ya Bikira Maria wa Rozari.

Kutokana na ushindi huo dhidi ya Waislam Baba Mtakatifu Pius V alianzisha rasmi Sherehe ya Mama Yetu wa Ushindi mwaka 1572. Mwaka 1573 Baba Mtakatifu Gregory XIII aliibadilisha jina sherehe hiyo na kuipa jina la Sherehe ya Bikira Maria Mama wa Rozari Takatifu.

Mwaka 1884 Baba Mtakatifu Leo XIII alitangaza rasmi kuwa mwezi wote wa kumi utakuwa mwezi wa kusali Rozari Takatifu akiwa na kumbukumbu ya ushindi ambao Wakristo waliupata dhidi ya Waislam katika vita vya Lepanto tarehe 7 Oktoba 1571. Lengo kubwa la kutangaza mwezi wa 10 kuwa mwezi wa Rozari lilikuwa kumweshimu na kumshukuru Mama Bikira Maria ambaye kwa maombezi yake Wakristo walipata ushindi Oktoba 7, 1571.

5. **Kwa nini Bikira Maria anajishughulisha na wokovu wa wanadamu?**

Bikira Maria alipalizwa mbinguni mwili na roho na kufanywa Malkia huko mbinguni. Kwa nini asikae huko akatulia na kuendelea kufurahia kumwona Mungu uso kwa uso? Kwa nini anawatokea watu duniani? Jibu ni rahisi sana:

Kwanza, Bikira Maria, kwa kumuona Mungu kama alivyo, anafahamu furaha isiyo na kifani ya kumwona Mungu na anataka kila mtu apate furaha hiyo; na ndiyo maana hawezi kutulia mbinguni kwa kuwa anatamani kila mmoja aionje furaha hiyo hasa wakosefu.

- Ndiyo maana anapowatokea watu duniani anatoa ujumbe kwa watu kufanya toba, kusali rozari, kupokea mateso kama njia ya kupata wokovu, kuombea marehemu wa toharani na kuonya wakosefu kubadili matendo yao. Pili, Bikira Maria anajishughulisha na wokovu wa wanadamu kwa kuwa alikabidhiwa jukumu hilo na mwanaye Yesu Kristo "Mama! Tazama, huyo ndiye mwanao" (Yoh. 19:26). Sisi sote tunawakilishwa na Yohane; sisi sote ni wana wa Maria. Hivyo Yesu hapa anamaanisha "Mama! Tazama, watoto wako". Neno "Tazama" lina maana kubwa sana: kututunza, kutushughulikia na kutuangalia kwa namna ya pekee. Hivyo Bikira Maria anaendelea siku zote kututunza, kutushughulikia na kutuangalia kwa namna ya pekee kwa maombezi yake ya kimama, kwa kutuelekeza nini tufanye pindi anapotokea kwa baadhi ya watu.

6. **"Tazama, huyu ndiye mama yako" (Yoh. 19:27)**
   - Yesu anamwambia Yohane amtazame mama yake (Bikira Maria). Yohane anatuwakilisha sisi sote. Sisi sote tumekabidhiwa kwa Bikira Maria kama Mama yetu. Je, tumtazameje Bikira Maria? Tutamtazama Bikira Maria kwa kumpenda, kumheshimu na zaidi ya yote kwa kusali Rozari Takatifu ambayo kiini chake ni tafakari ya mafumbo juu ya maisha ya Yesu na Bikira Maria. Kwa nini tusali Rozari?



   - Je, Rozari ina faida gani?
   - **Rozari inatuwezesha kuwa na ufahamu kamili kuhusu Yesu siku kwa siku**
   - **Rozari inatakasa roho zetu**
   - **Rozari inatupatia ushindi dhidi ya adui zetu**
   - **Rozari inatuwezesha kuishi maisha ya fadhila**
   - **Rozari inawasha ndani yetu moyo wa mapendo kwa Bwana Wetu Yesu Kristo**
   - **Rozari inatutajirisha kwa neema na mastahili**
   - **Rozari inatuwezesha kupata yale tunayohitaji kutoka kwa Mungu**
   - **Rozari inawezesha kufunguliwa kwa roho zilizopo toharani.**
   - **Rozari inatutia nguvu tuwapo katika madhaifu na changamoto za kimwili na kiroho.**

7. **Matokeo ya Kusali Rozari**
   - Kwa hakika Rozari ni sala yenye nguvu sana. Ukijiwekea mazoea ya kuisali utaona uzuri wa Rozari na kamwe hutaiacha. Zamani niliona kusali Rozari ni mzigo, ni kupoteza muda na kama kero tupu.

Lakini kila siku nazidi kuonja uzuri na nguvu ya Sala ya Rozari. Muda mzuri wa kusali Rozari ya binafsi, kwa kadiri ya uzoefu wangu binafsi, ni alfajiri kwani akili huwa imetulia sana. Hata hivyo, kila mtu anaweza kutenga muda wake atakaoona unafaa kwake. Kwa njia ya kusali Rozari:

- **Wadhambi wanasamehewa**
- **Roho zenye kiu zinaburudishwa**
- **Magumu yanafanywa kuwa mepesi**
- **Wanaopitia majaribu wanapata amani**
- **Maskini wanapata msaada**
- **Wenye mahangaiko wanapata faraja**
- **Roho za marehemu toharani zinapunguziwa mateso na zingine kufunguliwa**

Ee Mama Mpendelevu sana, utujalie nguvu ya kuweza kusali Rozari Takatifu kwa ajili ya wokovu wetu na wa dunia nzima, Amina.

Mama Bikira Maria alitoa ahadi 15 kwa yule au wale watakaosali Rozari takatifu kila siku. Ahadi hizi aliwapa Mtakatifu Dominic na mwenye heri Alan de la Roche.



1. Yeyote yule atakayesali kwa imani rozari hii takatifu atapokea neema kuu zenye nguvu
2. Naahidi ulinzi wa kipekee na neema za kipekee kwa yule atakayesali rozari hii
3. Rozari itakuwa silaha kubwa dhidi ya nguvu za kuzimu, itaharibu maovu, itapunguza dhambi na kushinda kutofautiana
4. Itafanya fadhila kukua, kazi nzuri kuongezeka, itapatia roho huruma tele toka kwa Mungu, itaondoa hamu ya wanadamu kupenda mambo ya dunia na majivuno yake na kufanya wapende zaidi mambo ya mbinguni. Ooh, ni kwa namna gani roho hizo zitajifurahisha na kubarikiwa kwa namna hii.
5. Roho zitakazojikabidhi kwangu kwa njia ya kusali rozari, kamwe hazitapotea.
6. Yeyote atakayesali rozari kwa uaminifu huku akiyatafakari matendo makuu ya rozari, kamwe hatashindwa na ubaya. Mungu hatamwadhibu katika hukumu yake, hatapotea katika kifo asichopangiwa na atabaki katika neema za Mungu na kustahili kupata uzima wa milele.



**Rozari Takatifu ni Ibada Muhimu**

7. Yeyote atakayekuwa mwaminifu katika kusali rozari, kamwe hatakufa bila ya kupokea Sakramenti takatifu za Kanisa.
8. Wote watakaokuwa waaminifu katika kusali rozari watadumu katika mwanga wa Mungu katika maisha yao na saa yao ya kufa na kupata neema zake tele; katika saa yao ya kufa watashiriki fadhila za watakatifu waliopo peponi
9. Nitawatoa toharani wale wote waliokuwa waaminifu katika kusali rozari
10. Watoto wangu waaminifu katika kusali rozari watapata fadhila kuu ya utukufu Mbinguni.
11. Utapata yale yote unayoniomba kwa kusali rozari
12. Wote wale wanaoeneza rozari hii takatifu nitawasaidia katika mahitaji yao
13. Nimepata toka kwa mwanangu Mtukufu kuwa mawakili wote wa rozari takatifu watapata waombezi toka baraza lote kuu la Mbinguni wakati wa maisha yao na wakati wa saa yao ya kufa.
14. Wote wanaosali rozari hii takatifu ni wanangu, na kaka na dada wa mwanangu wa pekee YESU KRISTO
15. Ibada kwa rozari takatifu ni ishara kuu ya kuelekea ukombozi

**16. Rejelea:**


1. https://www.radiombiu.co.tz/historia-fupi-ya-rozari-takatifu/
2. Padre Kelvin Onesmo Mkama, Jimbo Kuu la Mwanza (0753 266 330)
3. Askofu Method Kilaini, Msimamizi wa Kitume wa Jimbo la Bukoba – Kipindi cha Radio Maria na Ushirikiano na Mbiu Oktoba 8, 2023 Saa 12:30 Jioni
4. Mswada wa Kitabu cha Bikira Maria na Vijana (Daniel Benno Msangya, 2022).

# NDIVYO YALIVYO MAISHA

## Kwanini Lazima Tujifunze Kuwaamini Vijana?



**Daniel B Msangya**

"*Amua tu kuwa mpole, mwenye huruma, upendo, mtulivu na mwepesi kwa vijana, uwe mwema kwa wazee, waunge mkono wanaojitahidi na kuwa mvumilivu kwa wanyonge na wenye makosa. Wakati fulani katika maisha unapaswa kuyaishi yote hayo*," ndivyo anavyosema mwandishi maarufu wa vitabu vya kisaikolojia Lloyd Shearer.

Mimi pia nilifikiria haya, nilipohudhuria msiba wa baba yake rafiki yangu wa utotoni. Katika enzi za uhai wake tena wakati akiwa na nafasi yake katika jamii, alikuwa mtu anayejiweza kiuchumi. Wajihi wake, mrefu na mtu wa miraba minne. Wengine huita pandikizi. Tulimwogopa na kumhusudu. Ujasiri wake, umaarufu wake, mchango wake katika jamii na malezi bora ya familia yake. Hata hivyo, alikuwa mkali. Tulimpenda na kuiga mwenendo wake, sauti yake na tabia zake. Akitoka tuliigiza mwendo na sauti yake, tulitamba mbele ya watoto na hatimaye vijana wenzetu.

Alikuwa hodari wa mieleka kijiji kizima. Wanaume na wanawake walimhusudu. Aliporejea nyumbani tulifyata mikia. Alikuwa mtu wa kufoka na kutoa adhabu palepale.

. Hatukuamini kuona mikono yake yenye nguvu, iliyochapa kazi barabara, iliyotumika kutuchapa fimbo nyingi na kutuelekeza mambo ya kufanya, eti sasa mikono hiyo ilikuwa imefyata kifuani, imelegea, haiwezi tena kubeba mkongojo na mdomo wake alioutumia kukemea wavivu na wakorofi sasa hauwezi kutamka kitu.

Lakini tungelia kwa nini ikiwa tulimuona mkali na mwonevu? Alikuwa mtu gani hadi leo tumlilie? Sasa tunajikumbusha maneno yake tuliyochukia. Alikuwa anatuudhi, tena hakuwa na huruma maana hata kama jua ni kali ataagiza msikae bila kazi. Alitamani kuona tunaokota takataka, (alichukia mifuko ya plastiki iliyozagaa hovyo), alitaka tulime au kupalilia miti ya mbao na matunda. Alitaka kuona kila wakati umebeba jembe au kitabu unasoma au kuandika kazi za shuleni.

Inakuwaje tena sasa kwamba hatutasikiliza sauti yake nzito ya kutetemesha watoto wakorofi? Tulipita na rafiki yangu mbele ya jeneza na kutoa heshima za mwisho, tukitambua na kuthamini mchango wa malezi yake. Tuliyakumbuka mengi yaliyopita kwa mtiririko wa matukio ya utoto na ujana wetu. Tulijiuliza swali kuu: Bila huyu mfalme sisi tungekuwa wageni wa nani duniani? Tayari tulikuwa wazazi tena watoto wetu wameanza kupambana na maisha yao. Wengine bado wapo vyuoni, wengine wakihangaika na bahasha mkononi wakihaha kutafuta ajira. Tulijiuliza ikiwa watoto wetu wanalo jambo hata moja waliloiga kwetu sisi wazazi wa kizazi kipya. Je, wangeiga nini ilihali hatukai nao? Muda wote tumetingwa na kazi, safari ndefu na mambo ya ulevi.

Je, wanatuchukia, wanatupenda, wanatushirikishaje changamoto na mafanikio yao? Au wametubandika lakabu wanazojua wenyewe? Chapombe, Useless Dady na mzee wa vituko na majina mengine taja mwenyewe.

Ipo simulizi moja ya kale kutoka kwetu (Ingri Juu) kuhusu mkulima mmoja ambaye alifikia umri wa kuzeeka, akachoka na kuamua kukaa kwenye kibaraza chake. Hawezi kurudi tena kondeni kuendelea na kilimo.

Watoto wake walirithi mikoba yake wakawa wakipiga kazi shambani wakishindana bila kutegea. Kila mara walirudi na kumkuta mzee wao amelala pale kibarazani. Kadri siku zilivyosonga, walimuona mtu mvivu, asiyefaa kitu. Walimpa jina la Kiingereza: Useless Dady. Maana hafanyi kitu, walimuita "mzee wa kula kulala." Kijana mmoja mwenye hasira alikuwa amechoshwa na tabia hii ya baba yake. Akaamua kutengeneza jeneza kisirisiri. Akalivuta hadi pale kibarazani na kumwambia baba yake kuingia ndani ya jeneza. Bila kusema kitu, mzee wa watu aliinuka na kuingia ndani. Baada ya kufunga kidirisha cha usoni, kijana Yule alikokota jeneza hadi kwenye kingo za shamba, mahala penye bonde na korongo refu la kutisha. Lilifanana na Shimo refu lenye viumbe wakali wa kutisha




Mheshimiwa Padri Benedict Luzangi, Mratibu wa Idara ya Utume wa Vijana Jimboni Musoma

Kabla ya kusukuma lile jeneza aliona nuru kama mpasuko wa radi iliyopiga kutoka mbele ya uso wake. Kufumba na kufumbua kidirisha cha jeneza kilifunguka. Akamuona *Mzee Useless* akiwa hai, amelala kwa utulivu na tabasamu lake. Baba yake aliinua macho na kumwangalia kijana. "Najua unataka kunisukumiza kwenye makorongo nikafie mbali, lakini mwanangu, naomba kabla hujafanya hivyo, nipendekeze jambo moja". Alisihi mzee wa watu.

Kijana Yule alishangaa kidogo akauliza "Jambo gani. Wewe kikongwe?. "Nitoe kwenye jeneza hili ni zuri sana. Nisukume mwenyewe korongoni. Hili jeneza huenda likakusaidia kuzika watoto wako au kawape watoto wako watalihitaji kwa matumizi yao na kizazi chao. Kama hawataki peleka manispaa," aliongeza akitabasamu.

Maisha yanakwenda mbio tena kwa kasi kama mshale. Kwa mwendo wa kufumba na kufumbua. Dakika sifuri unakuwa mtoto, mara kijana tena mwanafunzi, kisha mwendabure, mtukutu, mlevi, unajisikia kuwa huru, kujaribu hiki na kile, kusoma, kucheza, kukaa kijiweni, kuonja vitu vikali, kabla hujamaliza uzee kuna mengi.



Padri Michael Nyamhanga, Msimamizi wa Parokia ya Ingri na Mlezi wa Vijana. Viongozi wote wa Vijana wanabeba dhamana ya malezi na maendeleo ya Sekta ya Vijana Jimbo la Musoma

Unapitia majaribu, unakwepa mishale, na ajali - unasogelea majukumu mazito na kabla muda haujapita unapoteza mwelekeo, unayumba, unarudi kwenye mstari na hatimaye unaingia daraja takatifu au la utume, umahiri kazini na mwisho la ukongwe. Kwangu ukongwe ni daraja hadimu. Wangapi wanalifikia? Wapo waliojaliwa, wakafika mwisho na wengi wameishia njiani. Wapo waliopotea wangali watoto, malaika, vijana wa kike na kiume…tena kwa magonjwa yanayozuilika….kwa ajali na majanga yanayozuilika; ilimradi hawakufikia daraja la uzee. Dunia inaomboleza sana! Je, hawakuheshimu wazazi kutimiza amri ya nne…upate heri na miaka mingi duniani? La, hili tumwachie Mwenye Mamlaka ya Juu.

Kwa waliofika sasa wanakazi moja - kusimulia hadithi ndefu za maisha yaliyopita. Je, yajayo hayawahusu? Maana vijana wanadai muda wa wazee umeshapita. Je, wako sahihi au wanapotoka? Wape nafasi wajadili.

Tunajua hiki ni kizazi cha teknolojia na sayansi. Vijana wanakuwa ndani ya kizazi cha simu janja, mitandao ya kijamii, vyombo vikongwe vya habari (magazeti, radio na runinga). Ni dunia ya utamaduni mpya, uliobeba takataka na vimelea vya magonjwa ya afya ya akili na roho. Vijana hawana heshima tena kwa wazee wao. Watoto wanakalia viti kwenye magari wazee wamesimama. Hata kanisani na majumbani. Wengine wanafanya njama kuwaua wazee ili kumiliki mali za urithi. Wanatamani wazee wajengewe vituo na kulundikwa huko kama wafanyavyo wazungu. "Kisha watuandikie kadi za Krismas eti wanatupenda," analalama mzee Madebo mwenye umri wa miaka 87.

Anasahau kuwa baadhi ya wazee vilevile wameteleza. Wanasema *"Uzee unaishia Ziroziro, mjini hakuna wazee." Ndiyo wapo wenye matatizo ya afya ya akili.*

Nani alaumiwe? Tunafikiri nini vijana wenzangu. Itakapofika zamu yetu kuwa wazee tutasemaje? Unasahauje kuwa mzee wako ndiye aliyekurithisha shamba unalolima, eneo unalokaa, elimu uliyopata, malezi na mahitaji yako ya chakula, makazi, malazi na mavazi yaliyokufikisha hapo ulipo tangu ulipokuwa mchanga?

**Swali kwa wazee na vijana**: Nani chanzo cha mmong'onyoko wa maadili? Kuna usemi wa kuku na yai nani alianza? Ndivyo ilivyo leo? Wazazi wanalalamika watoto na wajukuu kuwatelekeza, kukosa maadili na nidhamu. Wanalalamika watoto wa kizazi hiki hawajali wazazi wao, hawaheshimu wazee. Nyie vijana, wazee na walezi/wazazi mnasemaje? Nani wenye makosa? Wazee au vijana? Je, tukae kimya? Tunafanya nini kuwalea vijana wetu?



Baadhi ya Vijana wa Jimbo la Musoma (VIWAWA) wakiwa na viongozi walezi wao walipokutana Parokia ya Butiama hivi karibuni

Jarida hili linaalika Mjadala bila kujali ni mrefu na wala haujaanza leo. Lakini tuanzie hapa.

Nataka kuwaalika tushirikiane kuurejesha mjadala chini ya mwongozo wa ubunifu, kuja na majibu sahihi, tufanyeje? Maneno 1000 hadi 2000 yatapata nafasi.

Bila shaka mjadala utasaidia watafiti, wachungaji, walimu, walezi, wazazi, vijana na watunga sera kuokoteza habari za kuwasaidia vijana wa kizazi kipya. Tunataka wadau waje na maoni ya kuheshimiana, yanayoheshimisha wazee na wazee kuwapenda vijana, kuwaamini, ndivyo maisha yanavyokwenda na ndiyo dunia tunayoitaka. Kama sisi tulivyoaminiwa na wazee wetu wakajitolea, wakafa maskini ili sisi tuinuke, tusome, tupate familia zetu, tufikiri zaidi. Tutaepuka dhambi ya uzembe wa kufikiri na kutotimiza wajibu. Tutaepuka dhambi ya wizi wa fadhila, na utapeli wa ujambazi wa wazi kwa maendeleo ya kizazi cha sasa na kijacho. Ni mzunguko wa maisha. Mungu atubariki sote. Kila mtu atimize wajibu wake na kufikia ndoto yake. Wakatabahu!

**Mwandishi wa makala haya ni Mlezi na Mkufunzi wa Vijana wa Kituo cha Community Alive Musoma (CAM) na Taasisi ya Vyombo vya Habari Vijijini (ARUPA). Anapatikana kwa barua pepe: benno.apondo@gmail.com Simu: (0755893303).**

# BURUDANI NA MICHEZO

## Ushairi na Mshairi

| Eee Mungu Wape Tuzo Yao<br>Dan Benno Msangya, (*Lakabu ya Mshairi: Tai wa Mara*) | |
|---|---|
| 1. Leo ninawapa pole, ni pole ya kuumia<br>Wamisionari wapole, Tumepoteza mamia<br>Walitangulia wale, wenye malengo na nia<br>Walotangaza Injili, Mungu wape tuzo yao | 2. Mola wapokee pema, waangazie na mwanga<br>Wapumuzike salama, wapishane na majanga<br>Wape baraka na neema, Wachungaji na waganga<br>**Walotangaza Injili, Mungu wape tuzo yao** |
| 3. Walifundisha amani, walileta Neno Jema<br>Kutoka ughaibuni, walihubiri neema<br>Waliifundisha dini, ya wokovu na uzima<br>Walotangaza Injili, Mungu wape tuzo yao | 4. Wengi wamepukutika, kwa maradhi na ajali<br>Wengi walisha zeeka, kazi zao ni asali<br>Wengi wameshatutoka, kwa mapenzi ya jalali<br>**Walotangaza Injili, Mungu wape tuzo yao** |
| 5. Wachache nitawataja, Mapadiri na masista<br>John Kesi namtaja, James Lear nakuita<br>Mary Reese mwenye tija, mauti yamemkuta<br>Walotangaza Injili, Mungu wape tuzo yao | 6. Twakulilia watoto, wakubwa nasi vijana<br>Wasichana wenye wito, mazuri waliyaona<br>Uliyafanya mazito, huduma zilizofana<br>**Walotangaza Injili, Mungu wape tuzo yao** |
| 7. Mary Reese nakutaja, ulotutoka majuzi<br>Daima Sala na Hija, milele tutakuenzi<br>Kwa sifa zako za haja, umetuacha kipenzi<br>Walotangaza Injili, Mungu wape tuzo yao | 8. Miaka mia kutimiza, Mungu alikujalia<br>Kazi ulizitimiza, majonzi nakulilia<br>Mengi uliyowajuza, wanawake wanalia<br>**Walotangaza Injili, Mungu wape tuzo yao** |
| 9. Siyo kwa upendeleo, wengi walifanya mengi<br>Mengi ya maendeleo, yenye faida kwa wingi<br>Yanayofaa kwa leo, na siku zijazo nyingi<br>Walotangaza Injili, Mungu wape tuzo yao | 10. Wote hutuwezi taja, watawa na wakleri<br>Wenye sifa zenye tija, Tuombe wawe na heri<br>Wa imani mashujaa, Walimu wetu mahiri<br>**Walotangaza Injili, Mungu wape tuzo yao** |
| 11. Walifundisha injili, shuleni na kanisani,<br>Waliuliza maswali, kwao wakatekumeni<br>Toa kwa hali na mali, walitutoa gizani<br>Walotangaza Injili, Mungu wape tuzo yao | 12. Kilio kimetusibu, Jimbo letu la Musoma<br>Tumepoteza mababu, mashujaa walovuma Waliandika vitabu, wakakajenga na maboma<br>**Walotangaza Injili, Mungu wape tuzo yao** |
| 13. Kwa mengi twawakumbuka, tuwaenzi viongozi<br>Maaskofu wasifika, Rudin mtangulizi<br>Mayala alitutoka, naye Samba twawaenzi<br>Walotangaza Injili, Mungu wape tuzo yao | 14. Kazi waliitimiza, kuitangaza Injili<br>Leo tunaendeleza, shime kwa hali na mali<br>Kwa imani tunaweza, tumeshapewa akili<br>**Walotangaza injili, Mungu wape tuzo yao.** |

# MICHEZO NA WACHEZAJI

**Je, Wajua? Kombe la Jubilei ya Miaka 75 ya Kanisa Katoliki Jimbo la Musoma 1985 -1995)**; liliendeshwa na Chama cha Vijana Wakatoliki Wafanyakazi Jimboni (VIWAWA)? Je, wajua Timu za soka za VIWAWA zilizofika Daraja la Pili ?

Tuanze na Kombe hilo lililodhaminiwa na Askofu Mkuu Anthony Malaya akiwa Askofu wa awamu ya pili wa Jimbo la Musoma. Askofu mwenyewe alinunua Kombe hilo kwa thamani ya shilingi 20,000/- sawa kabisa na shilingi milioni 20 za sasa. Kombe hilo lilinunuliwa Nairobi, Kenya na kushindanisha Timu za Mkoa wa Mara na Mkoa wa Mwanza hasa Wilaya ya Magu iliyobeba Kombe hilo mara mbili mfululizo. Timu nyingine zilizoshiriki ni Polisi Mara, Chipukizi ya Parokia ya Mugumu (maarufu CHIPUKA FC) kutoka Serengeti, VIWAWA MUSOMA, Tarime Warriors, Afya na Majimaji zote za Shirati na Kipingi FC ya Kijiji cha Ingri Juu.

Mgeni rasmi wa kwanza katika ufunguzi na kilele cha michuano ya Kombe hilo alikuwa Mhashamu Askofu Anthony Mayala Septemba, 1985 miaka 3 kabla ya kuhamia Jimbo Kuu la Mwanza.



TIMU YA SOKA YA VIWAWA MUSOMA MJINI, 1993, PICHA KWA HISANI YA MAKTABA BINAFSI /DAN.)

**Je, Wajua? Bendi ya Mara Jaz**: Je, wajua? ilikuwa chini ya Parokia ya Komuge? Bendi hiyo ilivuma kati ya mwaka 1967 hadi 1975. Makao makuu ya Bendi awali yalikuwa Parokia ya Komuge na baadaye yalihamishiwa katika Mtaa wa Kennedy, Mjini Musoma na ikiongozwa na Marehemu Musomi Bwana. Bendi hiyo ilianzishwa na vijana wa Parokia ya Komuge na vyombo kufadhiliwa na Padri Wille Arthur, MM aliyekuwa paroko na mwasisi wa Parokia na Chuo cha Ukatekista cha Komuge. Miaka ya 1980 Bendi hiyo ilifufuliwa ikimilikiwa na mtu-binafsi na Musomi Bwana. Ni mojawapo ya matunda ya Wamisionari wa Maryknoll chini ya Paroko wa Komuge Padre Arthur Wille wakati huo. Baadhi ya nyimbo zilizovuma za Bendi hiyo: *Nataka kitenge uninunulie na kama hutaki nitakushitaki. Je, unakumbuka nyimbo zingine?*




Sisi ni wasanii wa Brass Band ya Shule ya Wasichana ya Kowak, tunapendeza katika picha ya pamoja na Baba Askofu wetu Michael Msonganzila

***Hata kwenye michezo na taaluma tupo vizuri***



Wakionesha kombe lao waliloshinda!
Wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Kowak, Rorya, Mara.

# ALAANI MAUAJI YA KIKATILI YA MWANAMICHEZO ANGELO MALIMA

**Na Veronica Vedasto, Musoma__________________Kiongozi mmoja wa Kanisa Katoliki Jimboni Musoma amelaani vikali wimbi la mauaji ya kikatili yanayosababishwa na watu wanaojifanya kuwa na hasira kali na wanaojichulia madaraka mkononi.** Padri Benedict Mukama Luzangi amelaani kitendo hicho wakati wa homilia ya Misa ya Marehemu Angelo Malima kijana Mkatoliki (Mwanaviwawa) kutoka Parokia ya Kristo Mfalme Rwamlimi Jimbo Katoliki la Musoma ambaye alifariki dunia baada ya kuchomwa na kisu sehemu ya moyo wakati akidai haki yake, kutokana na kuibiwa mara kwa mara. "Hapana. Hapana. Tunahitaji wakati fulani kuwa na moyo wa subira, tena hatupaswi kufumbia macho mauaji haya na wala hatuungi mkono kabisa tunalaani vikali, hata kama mtu mtatofautiana katika majibizano, msijichukulie sheria mkononi, lazima tuwe na mazungumzo yanayoleta amani, hata kama tutatofautiana katika fikra zetu na sio kuleta madhara ya kupoteza uhai wa mtu," amelaani vikali Padri Luzangi. Padri Luzangi amewaomba wanajumuiya na waamini wote kuwa na mahusiano mazuri baina yao, na kuacha tabia ya kulipiza kisasi au kujengeana chuki jambo ambalo sio zuri na jema, bali wanapaswa kuwa na mzungumzo ya kirafiki hata kama unataka kuminya haki ya mtu basi jitahidini sana msilete madhara ya mauaji, tumuombe Mungu atuepushe na moyo wa namna hiyo.



***Mwanasoka Marehemu Angelo***

Akisoma wasifu wa marehemu Angelo George Malima kaka wa marehemu Josephati Malima amesema marehemu Angelo mnamo Septemba 8, 2023 majira ya saa mbili usiku mita 20 kutoka nyumbani kwao alichomwa na kisu sehemu ya moyo na vijana waliosadikika kumuibia nyavu zake ziwani, na katika majibizano yao ndipo mmoja alipofanya unyama huo na kupelekea kuvuja damu nyingi.

Amesema walimkimbiza katika Hospitali ya Mkoa wa Mara ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Kwangwa wakati wanaendelea na jitihada za kutaka kuokoa maisha yake lakini Angelo Malima alifariki dunia kabla ya kupata huduma.

Akizungumza kwa niaba ya familia, Padri Peter Malima aliyekuwa likizo nyumbani baada ya kurejea kutoka masomoni, amewaomba waamini kuendelea kumuombea ndugu yao marehemu Angelo Malima ili apate pumziko la milele mbinguni. Aliwaombea jamaa, marafiki

na ndugu wenye mapenzi mema waliobaki kwani alisema ni kipindi kigumu sana walichonacho na bila neema ya Mungu peke yao hawawezi kitu.

Angelo George Malima ndio kijana wa kwanza

**Kabla ya kufikwa na mauti: Angelo Malima hakujua siku na saa yake**

aliyehamasisha michezo kwa viwawa katika Parokia ya Rwamlimi na alikuwa ni mchezaji wa mpira katika Timu ya Baruti FC,Biashara United ya Mkoa wa Mara na Tunduru



Masasi Kusini, ambapo alifanikiwa kuleta vikombe vingi vya ushindi katika timu hizo .




BWANA AMETOA NA BWANA AMETWAA JINA LA BWANA LIHIMIDIWE AMINA!

# HABARI KATIKA PICHA



Huruma na upendo: Mhashamu Askofu Liberatus Sangu wa Jimbo la Shinyanga akiwa amewapakata mawatoto wawili wa mazingira magumu, waliokotwa baada ya kutelekezwa na mama zao majalalani.







Baba Askofu Michael Msongonzila na Watumishi wa Altareni na viongozi wa Parokia wakiongozwa na Baba Paroko. Picha ya Pili: Askari mazoezini: Kila wakati ni mazoezi na kujiweka tayari kupambana dhidi ya maadui wanaotishia usalama wa raia na mali zao.








Askofu akiwabariki kidato cha pili kwa ajili ya kuanza mitihani ya mock.    Mtoto akimnong'oneza jambo Askofu katikati ya Misa





**WAAMINI ZAIDI YA 370 WAMEPATA SAKRAMENTI TAKATIFU YA KIPAIMARA KATIKA PAROKIA TEULE YA KIONGERA**

## MAHAFALI SHULE ZA AWALI, MSINGI NA SEKONDARI ZA JIMBO 2023





WAHITIMU ST POPE JOHN II NYAMONGO    WAHITIMU MILENIA YA TATU MASONGA    WAHITIMU DARASA LA SABA ST MICHAEL SIRARI






WAHITIMU DARASA LA AWALI MILLENIA YA TATU MASONGA    WAHITIMU SHULE YA CHRISTI THE KING IRAMBA








Wahitimu Kowak girls 2023.

Wahitimu wa darasa la saba shule ya Millenia ya tatau Masonga 2023





Picha ya pamoja Paroko wa Parokia yKowak padre Cleophas Sabure na Msaididizi wake Padri Avitus Niegra

Blass bendi ya Kowak Girls




Wahitimu shule ya wasichana ya chifu Wazangi .






Wageni na wahitimu Nyegina Sekondari

Wahitimu kidato cha nne Nyegina Sekondari 2023.





Wanandoa waliotimiza Miaka 50 ya Ndoa wakiwa na familia yao katika picha ya pamoja na Baba Askofu Michael Msonganzila aliyewatunukia hati ya kumbukumbu ya Jubilei yao na Picha ya Keki maalum ya Jubilei ya Dhahabu ya Ndoa Kutimiza Miaka 50



**KITENGE CHA JUBILEI YA MIAKA 40 YA UPADRI WA MHASHAMU BABA ASKOFU MICHAEL MSONGANZILA**
a



Hii ni keki iliyofinyangwa kiufundi na kuchukuwa mchoro wa jengo la Ofisi ya Parokia ya Mwisenge iliyozinduliwa na Baba Askofu Michael Msonganzila hivi karibuni .

**(Habari zaidi ukurasa wa kwanza)**




**SISI VIJANA JEURI YA TAIFA NA KANISA: TUKO TAYARI KUONYESHA UFUNDI WETU TULIOPATA KUTOKA CHUO CHA VETA ST. ANTHONY NYAMIONGO, MAKOKO. NI SEHEMU YA MAFUNZO YA VITENDO KATIKA KARAKANA YA CHUO CHA UFUNDI CHINI YA JIMBO KATOLIKI LA MUSOMA.**



**WANAFUNZI KOWAK GIRLS WAKIWA NA ASKOFU MICHAEL MSONGANZILA**



**WANAFUNZI CHUO CHA ST ANTHONY MAFUNZO YA UPISHI.**


## MATANGAZO YA SHULE ZA KANISA KATOLIKI JIMBO LA MUSOMA








**LITTLE FLOWERS SEC/SCHOOL: KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA: 0758717904/0765515940/0762890442**




MILENIA YA TATU
PRE & PRIMARY SCHOOL
Shule ipo ndani ya Jimbo Katoliki la Musoma Katika Parokia ya Masonga na inasimamiwa na Incarnate Word Sisters.
Tunapokea watoto kuanzia Chekechea hadi la sita.
Waalimu na Walezi bora kwaajili ya mtoto wako.
Ada zetu ni nafuu na tunalipa kwa awamu.
USAJILI
Unaendelea
Wasiliana nasi
+255 752 026 622 or +255 689 747 690.